


Kanisa Na Hali Yake

 Ugonjwa usio wa kawaida wa mtoto wapaswa kukumbukwa asubuhi hii katika maombi, hivyo hakika sote tunataka kufanya hivyo. Madaktari hata hawaujui. Wameupa jina fulani, lakini nafikiri wamejitungia tu moja la kuupa, ha—hawakujua ilikuwa ni nini. Pia, bali Kristo anajua ni nini. Naweza kuwaambia ni nini, ni ibilisi, hilo ni kweli, Ibilisi. Jina lo lote wapendalo kumpa, mbona, hiyo ni shauri yao. Bali hivyo ndivyo alivyo, mnaona, pepo mchafu. Sasa hebu, wote pamoja, mara moja pamoja sasa, “Amini Tu,” kila mmoja sasa na aimbe.

Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Yote yatendeka, amini tu.

² Bwana atakuponya, dada. Tuombe kwa ajili ya msichana huyu sasa tukiinamisha vichwa vyetu.

³ Baba yetu wa Mbinguni, yaonekana siwezi tu kuliondoa akilini mwangu. Yule msichana mdogo pale, anakufa, ni kipenzi cha mtu fulani. Yeye ni kiumbe Chako, na Shetani anamnyang’anya maisha yake machanga. Naomba kwamba katika Jina la Kristo Wewe utauzuia mkono wa mauti, umrudishe nyuma adui yule. Wewe, Bwana, uwezaye kuifanya Bahari ya Shamu kujenga kuta pande zote mbili, na kuwapa wana wa Israeli, warithi Wako, safari ya salama kuvuka bahari na kuingia katika nchi ya ahadi. Mungu, leo tunaomba kwamba Wewe utaondoa kila pingamizi na kumwezesha mtoto huyu kuishi. Tumepewa kuomba. Na, sisi kama kundi la watu wanaokuamini Wewe, tunaomba katika Jina la Yesu kuponywa kwa mtoto huyu. Amina.

⁴ Leo ni kwa moyo uliojawa na shukrani ambapo na—naja kwenu tena katika Jina la Bwana Yesu. Nilifika nyumbani mapema tu kutoka Louisiana. Nikafikiri pengine kama ningalifika hapa kabla ya Jumapili ningeweza kuwa na shule ya Jumapili. Ndipo hali ya hewa ilikuwa ya joto sana kule, hata sisi. . . asubuhi hii ingalikuwa nafuu kidogo, baridi kidogo ukilinganisha na Louisiana. Usingeketi kamwe kwenye jengo kama hili bila ya pepeo, huko Louisiana, ingebaridishwa au ungelizimia.

⁵ Na kwa hiyo nimekuja ili nipate mapumziko ya siku moja mbili kabla ya kuondoka sasa moja kwa moja, kuelekea Saskatchewan ya Kaskazini, juma lijalo, na hiyo ni hadi Prince Albert. Hapo ndipo kikomo cha barabara ulimwenguni, kutoka upande ule mwingine. Unavuka sehemu yote ya nchi

bila barabara zo zote, na hakuna cho chote ila Wahindi na Waeskimo nyuma huko ndani ndani kupita sehemu ambayo huwa tunakwenda safari hii. Kwa hiyo tuna watu wengi watakaokuwepo kwenye mkutano huu kutoka kila sehemu ya Canada. Wanasema baadhi yao watakuja moja kwa moja kutoka Pwani ya Magharibi, watakuja huko. Nami hakika ninatamani maombi yenu enyi watu, kwamba Mungu atakutana nasi na kutupa mkutano mzuri mno, wenye baraka sana, kwa ajili ya utukufu Wake. Imepita kama miaka minne mitano tangu nilipokuwa kule Canada. Nami ninao marafiki wa kweli hasa huko, ambao ni watu wazuri sana.

⁶ Na kwa hiyo ni waaminifu sana kwenda kanisani. Haidhuru kuna baridi jinsi gani, watajifunika blanketi na kuketi kwenye gari la kukokotwa, na kupanda farasi kwa maili thelathini, wapate kufika kanisani. Watatembea kwenye chungu za theluji na kadhalika, vijana kwa wazee. Wote hujikusanya pamoja. Na jamaa moja inachukua nyingine na kuanza kutembea, na wanakwenda. Kujitolea kwao ndi—ndiko kunakowafanya wanufaike sana katika ibada. Pasipo kujitolea, ibada haina faida sana. Yakubidi kweli ushuke chini ukafanye jambo ambalo linaumiza sana, yabidi kuweka kando mambo fulani na kusimamisha kazi, na kufanya *hili* au *lile*, *ili* upate kwenda kanisani na kumwonyesha Mungu kwamba unampenda Yeye, na unapojitolea kwenda, hapo ndipo basi utapata kitu kwake.

⁷ Ni kama tu watoto wangu. Billy Paul, nilifikiri ninge... Mimi sikupata kitu nilipokuwa mtoto mdogo. Mama alikuwa akichukua pengine mfuko mmoja wa peremende akaugawanya, vipande viwili vitatu kwa kila mmoja. Pengine kwa Krismasi tungepata zomari ya bati au bastola ya fataki, au kitu fulani. Nami niliwaona watoto wengine na magari ya kukokotwa na baiskeli na kadhalika, nguo nzuri na jaketi nzito. Na mimi—mimi, ilinifanya nijisikie vibaya sana, nikasema, “Kama nikijaliwa kupata watoto wo wote wangu, nitawafanyia kila niwezacho.” Naam, ningekubali kukaa na njaa kusudi niwapatie watoto wangu kitu fulani. Basi nilipoishi... Billy alipokuwa mvulana mdogo tu, ningemnunulia baiskeli ndogo ya magurudumu matatu, nami ningempatia kila kitu. Na Meda angejaribu kila kitu, kujitolea kwa nguo zake mwenyewe na kadhalika, kumpatia kitu fulani. Lakini unajua tulianza kuona nini? Nilimnunulia baiskeli ndogo ya magurudumu matatu, na upinde mdogo na mishale, na kila kitu. Ningemkuta na ki—kijiko au kijiti, huko uwani, akichimba mahali fulani. Unaona? Nikasema, “Wanaofuata hawatakuwa namna hivyo.” Unaona? Ukimpa tu mtu ye yote kila kitu moja kwa moja mkononi mwao, hawakitaki. Ni jambo ambalo ingekubidi kujitolea kwake.

⁸ Na hivyo ndivyo ulivyo wokovu. Ni kujinyima kabisa. Ndiyo, Ndugu Roy. Ni—ni kujitoa ambako yakupasa ufanye kila siku, kitu cha—cha kumkaribia Mungu na kutenda kitu fulani. Nami

najua nyinyi nyote mmejitolea asubuhi hii, kuketi kwenye jengo hili lenye joto. Tunapoketi hapa, hebu tuweke akili zetu kwenye Kafara kuu zaidi ya zote ambayo binadamu aliwahi kupewa atoe, hiyo ilikuwa Yesu Kristo wakati Yeye alipopewa jukumu la kuja duniani kufa badala yetu. Isitoshe, nafsi Yake ilishuka kuzimuni na ikakaa mle siku tatu usiku na mchana, na siku ya tatu Yeye akafufuka, na sasa amepaa juu, ameketi mkono wa kuume wa Mungu, Mbinguni, akifanya upatanisho tunapokiri dhabihu Yake na neema Yake iliyotolewa kwa ajili yetu.

⁹ Sasa huko katika...huko juu ambako tunakwenda, watakuwepo watu wengi, maskini hohehohe, wasio na mbele wala nyuma, itabidi kuuza mmoja wa ng'ombe zao, kondoo zao wawili watatu, au kitu fulani, wapate kuhudhuria mikutano hiyo. Mzee wa Kiesikimo labda ataleta baadhi ya ngozi zake apate kuziua, ambazo alizihitaji sana kwa ajili ya jamaa yake, apate kuja. Mfanya biashara wa Kihindi itambidi afanye vivyo hivyo. Sasa, angalau tunaweza kuwaombea watu hao, sivyo? Na tunaomba kwamba Mungu atawapa jambo kubwa.

¹⁰ Sasa, kuna joto, sitaki kuwaweka kwa muda mrefu. Na nataka asubuhi hii tuelekeze nia zetu, kabla tu hatujawaombea wagonjwa, juu ya *Kanisa Na Hali Yake*. Na, sasa, naona kwamba siku chache zilizopita nilipewa Ujumbe kwa ajili ya kanisa huko Shreveport, Louisiana, na ni—ninaamini ni hali za kanisa. Nasi tutamwelekea Mungu kwa huo asubuhi hii, na kuomba na kumsihi Mungu atusaidie. Msikusudie kuchukua msimamo ule ule, bali msihini Mungu atusaidie katika siku hii ambayo tunaishi. Na kabla tu...Hii ni Biblia tukufu ya kale, bali mle ndani mna mambo ya Uzima wa Milele.

¹¹ Basi kumbuka, Neno ni Mungu, Mungu si zaidi ya Neno Lake. Nasi si zaidi ya neno letu, na kama tukifanya...Bila shaka, sasa, wewe na mimi kwa maana—maana nyingine, sababu twaweza—twaweza kusema, “Loo, nitafanya jambo fulani,” tunakusudia hilo moyoni mwetu, lakini hali zinaweza kujitokeza ambapo hatuwezi—hatuwezi kufanya jambo tulilosema tungetenda. Bali Mungu hawezi kufanya hivyo, kwa sababu Yeye hana kikomo na Yeye anajua kila kitu, na kila kitu kilichowahi kuwa, kitakuwa. Kwa hiyo, Yeye hawezi kutamka maneno isipokuwa Yeye anajua anaweza kuyatimiza.

¹² Ndipo Ibrahimu, wakati alipokuwa na miaka mia moja, aliyaita mambo yale yasiyokuwepo, kana kwamba yamekuwepo. Sasa ninasema haya kwa kuwapa moyo wale watakaoombewa, wagonjwa. Ibrahimu aliyaita mambo yale yasiyokuwepo, kana kwamba yamekuwako, akichukulia kwamba Yeye Ambaye alifanya ahadi aweza kufanya, au, kutimiza yale ambayo Yeye aliahidi. Sasa, Mungu alipomwambia Ibrahimu, alipokuwa na umri wa miaka sitini...sabini na mitano, na Sara alikuwa na sitini na mitano, kwamba watapata mtoto, mbona, ilikuwa haiwezekani kabisa. Naye aliamini hilo na akamtazamia mtoto

huyu, na akamhesabu yule mtoto kana kwamba kweli yupo, kwa miaka ishirini na mitano kabla mtoto hajaja. Naye Ibrahimu alikuwa na umri wa miaka mia moja mtoto yule alipozaliwa, na Sara alikuwa na tisini, kwa sababu alimwamini Yeye. Naye aliyaita yale mambo ambayo hayako, kana kwamba yako.

¹³ Sasa, hayo ni kwa ajili ya wagonjwa na wanaoteseka watakaombewa. Haidhuru matatizo yako ni nini, kama wewe u... una magonjwa ya namna gani, jinsi ulivyo na hali mbaya, unapomkubali Kristo, Neno Lake, basi unaita mambo ambayo yapo, kana kwamba hayakuwepo, kama yanapingana na Neno la Mungu. Sasa, Mungu alisema, “Kuomba kwa imani kutamwoko mgonjwa yule.” Vema, kama Mungu alisema hivyo, hilo latosha. Basi na tuweke nia zetu, tumaini, na tutende kana kwamba tayari imetendeka. Hilo tayari limeisha wakati tunapolikubali.

¹⁴ Wokovu ni vivyo hivyo. Tunauamini, tunaukubali, tunauamini mioyoni mwetu, tunaenda mbele za Mungu na kumkubali Kristo kama Mwokozi wetu binafsi, na kumkubali Yeye. Kama upo hapa asubuhi hii, na u mwenye dhambi, nawe hujaokoka, nawe unataka kuponywa, u mgonjwa, kwanza mtafute Bwana. Mkubali Yeye kama Mwokozi wako, halafu ugonjwa huo utaondoka kabisa. Hata iwe nini, hebu weka mawazo yako yote (kwa kila jambo ulilo nalo) juu ya Utu wote, Kristo Yesu, kila kitu kitakuwa sawa.

¹⁵ Kwa hiyo sasa weka nia yako juu ya jambo hilo, sababu nilisema maneno haya machache kwa ajili ya wale walio wagonjwa na wanaoteseka, kwa hiyo basi nitazungumzia asubuhi hii juu ya kanisa na hali ile. Kwani naona kwamba ingawa kuponywa kwa Kiungu ni kwa ajabu, lakini nilipokuwa kule Shreveport, nilifanya ibada tatu tu za kuponya nilipokuwa kule, tatu, au labda nne, zikizidi sana, katika siku kumi na moja. Ni muhimu zaidi kuhubiria nafsi za wanadamu kuliko kuchukua muda mwingi sana katika kuponya Kiungu. Ingawa, watu ambao ni wagonjwa na wahitaji, Mungu anaweza kuwaponya. Na imekwisha thibitishwa ulimwenguni kote, kwamba Yeye huponya. Lakini jambo lililo muhimu, sasa, ni kwa nafsi ambayo haitakufa kamwe. Mwili utakufa. Bali nafsi haitakufa kamwe, nasi yatupasa kushikilia kiwango hicho na kuwa waaminifu kwa Mungu.

¹⁶ Mara nyingi nimesema jambo hili. Nataka kila kitu kitendeke, lakini nifikapo pale mtoni asubuhi ile, sitaki kupata shida yo yote kule. Nataka niwe nimeshika tikiti yangu mkononi mwangu, nikingojea jina langu. Nami nataka kusema, kama Paulo wa kale, Ndugu Creech, “Namjua Yeye katika uwezo wa kufufuka Kwake.” Ili kwamba Yeye atakapowaita wafu, nitatoka... Nataka kumjua Yeye katika uwezo wa kufufuka Kwake.

17 Kwa hiyo, sasa, Yeye Ambaye Ndiye Mwandishi wa Kitabu hiki, hebu na tuviinamishe vichwa vyetu na mioyo Kwake kwa muda mfupi.

18 Basi, Ee Mungu, Baba yetu, tunakuja Kwako sasa, kuomba kwamba Wewe utatufungulia Neno Lako. Tungeweza kufungua kurasa, lakini ni Roho Mtakatifu pekee anayeweza kulifungua Neno. Kwa hiyo lifungue Hilo kwa ajili yetu asubuhi hii, Baba, na utupe wingi wa neema Yako. Twakungojea Wewe. Roho Mtakatifu na aingie katika Neno, na alitoe Hilo kupitia midomo ya binadamu kuingia miyoni mwa binadamu, pia na achukue Hilo na aliweke ndani ya kila moyo kulingana na mahitaji yetu. Na hizi ibada zitakapokwisha, tuko tayari kurudi manyumbani mwetu, tutainamisha vichwa vyetu kwa unyenyekevu na kukupa Wewe shukurani na sifa, kwa yote yale tuliyojifunza Kwako na yale Wewe umetutendea. Tunaomba katika Jina la Kristo. Amina.

19 Somo la Neno, katika Yohana Mt., sura ya 1, ninyi ambao mna Biblia na mngetaka kusoma pamoja nami au kuliandika kama somo. Nasi tutasoma kifungu hicho kutoka katika Neno, na halafu hebu tuombe, ya kwamba Roho Mtakatifu atachukua yaliyomo katika Neno atupe sisi. Tunaweza kulisoma Hilo, sisi ambao tuna uwezo wa kusoma tunaweza kusoma Hilo, bali ni Mungu pekee awezaye kuleta maana ya yaliyomo. Fungu la maneno linaweza kusomwa, sababu Hilo ni Neno Lake, lakini basi maana—maana ya yaliyomo hayana budi kutolewa na Mungu. Sasa, katika Yohana Mt., sura ya 1, na hebu tuanzie kwenye aya ya 28 na kuendelea kusoma hadi ya 32, yote pamoja.

Hayo yalifanyika...huko ng'ambo ya Yordani, alikokuwako Yahana akibatiza.

...siku ya pili yake Yohana amwona Yesu anakuja kwake, ndipo akasema, Tazama Mwana-kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimengu!

Huyu ndiye niliyenena habari zake ya kwamba, Yuaja mtu nyuma yangu ambaye amekuwa mbele yangu; kwa maana alikuwa kabla yangu.

Wala mimi sikumjua; lakini yeye...lakini kusudi adhi...afanywe dhahiri kwa Israeli, ndiyo maana nimekuja nikibatiza kwa maji.

...Yohana akashuhudia, akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake.

Nataka kusoma hilo tena, aya hiyo ya mwisho, aya ya 32.

Tena Yohana akashuhudia, akisema, Nimemwona Roho akishuka kama hua kutoka mbinguni; naye akakaa juu yake.

²⁰ Sasa Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Neno hilo. Nataka mjaribu ku—kushika kila neno kama tukiweza. Mnaweza kunisikia sawasawa huko nyuma kabisa? Sawa, mnaweza kunisikia huko nyuma? Kama mwanisikia, inueni mikono yenu juu. Hilo ni jema.

²¹ Sasa, nataka kuzungumza nanyi asubuhi hii juu ya—juu ya mfano, kwa njia fulani kwamba hata yule—yule mtu asiye wa kanisa kabisa na yumo humu ndani angeweza kuelewa. Sasa, tunakuja kanisani tupate kujifanya watu bora zaidi. Tunakuja kujifanya watu wazuri zaidi, Wakristo wazuri zaidi, raia bora zaidi, baba wazuri zaidi, mama mzuri zaidi, majirani bora zaidi. Tunakuja kwa sababu Kristo ametuambia kama tungkuja, tuombe lo lote katika Jina Lake, ambapo tumekusanyika pamoja kadiri ya wawili watatu, Yeye angekuwa pamoja nasi na angetujalia tuombayo. Kwa hiyo, ni nini kingekuwa zaidi, kingekuwa bora zaidi kwetu sisi leo kuliko kujua kwamba tuko kanisani kujiendeleza, kupanua ufahamu wetu. Wangapi wangesema, “Hilo ndilo lililonileta hapa?” Hebu tuone. “Na—nataka ufahamu bora zaidi.” Na hatuwezi—hatuwezi kuwa na ufahamu bora zaidi isipokuwa u- . . . Na kama tunataka kupata ufahamu wa Mungu, yabidi utoke kwenye Neno la Mungu, kwani Neno ndilo Mungu alitupa tupate kuzilisha nafsi zetu zenye njaa. Na Roho Mtakatifu alipelekwa ili kulichukua Neno la Mungu na kutulisha kwa Neno. Unaliona? Unaona, sisi. . . Roho Mtakatifu alitumwa kutoka kwa Mungu, kulichukua Neno la Mungu na kulitoa Hilo kwetu kulingana na haja zetu. Sasa, mimi ninafurahi sana kwamba Mungu alitengeneza njia kama hiyo. Na wewe je? Apate kutulisha sisi.

²² Sisi ni kondoo wa malisho Yake. Tutazungumzia jambo hilo hivi punde, kondoo. Na sisi tu viumbe vya Mungu vyenye sehemu tatu, na hapo Yeye awezapo kutwaa utawala kamili juu yetu anaweza kutuongoza na kutuonyesha njia.

²³ Sasa, ilimpendeza sana Mungu, hata wakati Yeye alipompeleka Yesu duniani, kwamba ilimpendeza Yeye kumwakilisha Yeye kama mnyama, na mnyama huyo alikuwa ni mwana-kondoo. Nyuma huko mwanzoni, katika Bustani ya Edeni, katika vivuli vilivyotangulia kuja kwa Yesu, Mungu alitoa dhabihu ya mwa—mwana-kondoo kuwa toleo la kusimama badala yake katika vivuli vya kuja kwa Kristo. Sasa, mara nyingi nimeshangaa kwa nini Mungu amwonyeshe Kristo hapo awali kama mnyama, kama hayawani. Bali tunakuja kuona kwamba Mwana-Kondoo, sababu ya Yeye kuchagua mwana-kondoo, mwana-kondoo ndiye mnyenyekevu sana na mpole sana kati ya viumbe vyote vilivyomo duniani. Hakuna cho chote kilicho kinyenyekevu zaidi na kipole zaidi ya mwana-kondoo mchanga, hana hatia, hajitegemei. Ha—hana kiburi. Yu kiumbe mdogo, mpole na mnyenyekevu. Na Mungu alipomwakilisha Kristo kwa ulimwengu, Yeye alimwakilisha Huyu katika mwana-kondoo.

²⁴ Sasa, bali wakati Mungu, Baba Mungu, Yehova, alipojiwakilisha Mwenyewe toka Mbinguni, Yeye aliwakilishwa katika ndege aliye mtiifu na mnyenyekevu sana kati ya ndege wote warukao angani, yaani, hua. Hakuna ndege aliye mpole kuliko hua. Nilifanya uchunguzi wa kutosha juu ya maisha ya ndege na wanyama wa porini, na hua ni ndege wa kipekee kati ya ndege ye yote arukaye angani. Hua ni mwe-mwe-mwenye upendo. Hua ni mpole. Na hua hana nyongo, ndiye ndege pekee katika jamii ya ndege ambaye hana nyongo. Hiyo ndiyo sababu humwoni kamwe hua po pote isipokuwa mahali penye punje na mbegu.

²⁵ Sasa, katika safina, alikuweco hua. Na hua amewakilishwa katika sehemu nyingi katika Biblia. Ni mfano wa Roho Mtakatifu. Na pia mwana-kondoo amewakilishwa katika sehemu nyingi za Biblia, kama Kristo, katika Ufunuo, tukirudi kule nyuma hadi Mwanzo, vivyo hivyo na hua.

²⁶ Na katika Kitabu cha Mwanzo, hua alikuwa katika safina, akikaa kwenye kiota pamoja na we—na ndege wengine wa angani; na mmoja wao alikuwa kunguru, kunguru. Na kunguru ni mmoja wa ndege wachoyo sana waliopo, kunguru na kunguru milio, nakisia, labda ndio ndege wachoyo sana tuwezao kuwapata. Kunguru ni ndege aliye na maisha marefu sana, naye huishi (wamedai) kwa, wakati mwingine, miaka mia mbili au mia tatu, huyo kunguru. . . Kasuku huishi zaidi ya hiyo.

²⁷ Bali hua ni mnyama mmoja au ndege mmoja ambaye hana nyongo. Sasa, kunguru angeweza kukaa hapa na ale mzoga. Hutamwona hua kwenye mzoga huo kamwe. Hawezi kuustahimili. Uvundo wake puani mwake, asingeweza kuvumilia. Ingemfanya mgonjwa. Hawawazi kabisa kuvumilia kitu cho chote ambacho kinaoza, kinachovunda. Hawawazi kukivumilia, kwa hiyo asingeweza kukila. Kama angekila, kingemuua hua mara moja, kwa sababu kile kinachoyeyusha chakula ni kufurika kwa nyongo tumboni ambako huyeyusha chakula. Na kama hakuna nyongo ya kuingia humo kutekeleza jambo hili, basi lingemuua hua. Kwa hiyo sikuzote utamwona hua palipo na kitu kisafi, kitu ambacho ni kizima.

²⁸ Sasa, kunguru ni tofauti. Naam, hebu angalia kunguru akiwa mfano wa mnafiki. Kunguru anaweza kuketi pale juu ya—juu ya mzoga na ale kiasi apendacho kula, kisha aruke moja kwa moja hadi shambani na ale ngano, pia. Bali hua hawazi kula ngano halafu aurukie mzoga.

²⁹ Kwa hiyo, mnafiki, mtu anaweza kuwa mnafiki na ale vyote viwili vitu vya kiroho, na vitu vizuri na vitu vibaya. Bali Mkristo hasa aliyezaliwa mara ya pili hawazi kuvumilia mambo mabaya, na anaweza tu kula kitu kizuri. Angalia hilo! Uonapo mtu ambaye anaweza kwenda kwenye dansi, atoke aende akalewe, atoke aende akaishi katika dhambi, arudi kanisani na pengine

apaze sauti kwa nguvu kama mtakatifu ye yote, jambo ni kwamba, yeye ni tai mzoga, anaweza kula vyote viwili kitu kilichooza na kitu kizima. Bali Mkristo hasa hawezi kustahimili mambo hayo tena, kwa maana amepita toka mautini kuingia Uzimani. Na mara lingemhukumu mno, hata mawazo tu ya jambo hilo, mpaka lingemhukumu mpaka angegeuza uso wake na kuondoka. Loo, ni picha iliyoje!

³⁰ Naam, mwana-kondoo ni jamaa mdogo na mpole sana. Hawezi, hawezi kujisaidia. Hajitegemei, kwa sababu hawezi kujisaidia mwenyewe. Hapa siku moja nilikuwa nikipita malishoni nilipokuwa mlinzi, nami nikamwona maskini mwana-kondoo mchanga, na wengine wote kwa namna fulani wamemwacha, naye alikuwa amezongwazongwa katika rundo la seng'enge. Na maskini jamaa huyo alikuwa amelala pale, anatokwa na damu na kulia. Nami nikasogea karibu na kuangalia mbali huko juu, kama nusu maili huko juu, kulikuwa na kundi zima la kondoo. Sasa, yeye angelala pale pale na kunguru mara moja wangeanza kumdonoa macho kama tusingalimtoa. Bali nilimfungua maskini jamaa yule, nikamchukua mkononi mwangu. Hakukataa kamwe. Alilala kimya kabisa. Nikamchukua mikononi mwangu. Kwanza—mara ya kwanza, labda, mwanadamu amewahi kumshika mikononi, lakini alikuwa mpole. Alikuwa tayari kuongozwa. Alikuwa tayari kusaidiwa. Natumaini mnalion. Alikuwa tayari kutojaribu kukataa au kupiga teke, au kuuma. Wana-kondoo hawapigi mateke, hawaumi; hujinyenyekeza tu. Na maskini jamaa huyu mdogo, nilimbeba na kumweka kwenye kondoo wengine. Mnamo dakika chache mama yake akamwona, jinsi alivyokuwa na furaha! Sasa, jinsi hilo lilivyo mfano halisi wa Mwana-Kondoo wa Mungu!

³¹ Unajua, mahali wanapokwenda kuwachinja kondoo, unajua anayewaongoza kondoo machinjioni, ni mbuzi. Bali mbuzi atamwongoza kondoo moja kwa moja hadi kwenye maporomoko ya machinjioni, na, mara akimfikisha kondoo kwenye maporomoko, basi ataruka nje. Lakini, loo, wao husema, wanapotaka kumchinja mbuzi, basi anaanza matata kwelikweli. Unaona?

³² Na hivyo ndivyo Ibilisi atatenda. Atajaribu kuongoza wana wa Mungu moja kwa moja hatarini, bali ufikapo wakati wake wa kufa, atafanya matata kwelikweli wakati huo. Hivyo ndivyo Ibilisi hutenda. Na hivyo ndivyo wakati mwingine, maskini msichana aliyejirembesha kipumbavu au maskini mvulana mhuni, akiwa na paketi ya sigara au chupa ya wiske, angemwongoza msichana mdogo vibaya, mwana-kondoo, akiwa na kitoto cha mtu, kwenye mambo mabaya. “Loo, yote ni sawa. Mambo hayo ya kujifanya mwema ya kanisa hayafai kitu.” Lakini acha kifo kimpige maskini mvulana huyo wakati mmoja,

utamsikia akilia kama paka na kupiga mayowe nchini kote. Na hivyo ndivyo Ibilisi anavyotenda.

³³ Bali mwana-kondoo ni mpole sana, hata anaweza kuongozwa. Na hiyo ndiyo sababu Mungu alimwakilisha Kristo kama Mwana-Kondoo, na Yeye Mwenyewe kama Hua. Basi siku ile ambayo Yohana alimbatiza Yesu kwenye mto wa Yordani, moja ya matukio makuu sana yaliyowahi kutukia, yalitukia papo hapo. Angalia jinsi linavyopendeza! Mwana-Kondoo, aliye mpole sana kati ya viumbe vyote vya duniani, na Hua, aliye mpole sana kati ya ndege wote wa Mbinguni. Sasa, ndiyo njia pekee ambayo wanguweza kuunganishwa. Ndiyo njia pekee ambayo Hua angeweza kuja juu ya Mwana-Kondoo. Sasa, Hua aliposhuka, Yohana alimwona Yesu, ndipo akasema, “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu, azichukuaye dhambi za ulimwengu.” Naye Yohana akasema, “Namshudia, nikimwona Roho wa Mungu kama Hua akishuka, akikaa juu Yake.” Haleluya! Ndivyo ilivyo. Hua na Mwana-Kondoo waliungana pamoja. Hapo ndipo Mungu na Mwanadamu walipokuwa mmoja. Hapo ndipo Mbingu na dunia vilipokumbatiana. Haleluya! Hapo ndipo Mungu alifanyika mwili, akaileta, hapo ndipo Mungu aliposhuka kutoka kwenye hali ya Roho akafanyika Mtu akakaa kwetu. Hapo ndipo Umilele wote ulipokumbatiana. Hapo ndipo taifa lililoanguka la watu wa Adamu na Yehova Mungu na kila malaika walipoungana, hapo Mungu na binadamu walipofanyika mmoja, kwenye siku ile kuu ya kumbukumbu Yohana alipombatiza Yesu.

Sasa, vipi kama wangukuwa mbwa mwitu? Ule mlio mtamu wa Hua hungeweza kumvumilia mbwa mwitu.

³⁴ Ni kitu gani kinapendeza kuliko kuwasikia kwenye machweo ya jua maskini hua wazee wamekaa kule wanaimba kidogo? Baada ya kumpoteza mke wangu na mtoto... Nisingemruhusu ye yote ajue nilichokuwa ninafanya. Nilizoea kuingia kwenye gari langu kuukuu, ningeliendesha kuvuka barabara hapa, nikatoka nikaenda hapa kwenye makaburi ya Walnut Ridge, nikaketi pale kando ya mti na kutazama chini kwenye kaburi. Nisingeweza kuwasahau hata kidogo. Ilionekana kana kwamba singeweza kuvumilia zaidi. Nafikiria mtoto wangu mchanga, amelala pale, mwenye umri wa miezi minane. Jinsi alivyozoea kuinyoza mikono yake midogo na kunifikia, nami ningepiga honi au kumwambia jambo fulani, naye angefanya “guu-guu,” huku akinyosha mikono yake midogo. Nami ningeketi chini kando ya ule mti, hasa sana inapofikia wakati wa jioni. Na kulikuwepo na hua mzee ambaye alizoea kukaa nje kule kwenye kichaka, akaanza kuimba. Loo, jamani! Wakati mmoja nilishangaa kama ilikuwa ni nafsi isiyopatikana na mauti ya mtoto wangu inarudi kujaribu kuzungumza nami. Hakuna kilicho kitamu kuliko kule kuimba kwa hua. Jinsi alivyo na upendo! Huleta habari njema. Jinsi

anavyojaribu kuleta amani! Amka asubuhi na mapema, nenda nje huko kwenye vichaka karibu na mahali ninakoishi, ni jambo la amani jinsi gani kusikiliza! Wakiketi kule juu kwenye ule mti mrefu mno, wale hua wakiimbiana.

³⁵ Hivi majuzi, kule kwa Ndugu Cox, kizee mama hua alikuwa na makinda wadogo wawili. Nao walikaa juu kabisa kwenye kilele cha jengo, ili kwamba paka wasiweze kuwapata. Na maskini mama hua angewalisha. Kisha angeshuka na kuwachukua na kuwafanya wapande juu mtini, nao wangeketi pale wakiwa wamepitishana shingo zao mmoja kwa mwingine, na kuimba na kubembelezana, mchana kutwa, maskini makinda wawili wadogo na wapole.

³⁶ Basi nikafikiria ambavyo Mungu, (hua ni ndege mwenye kupendana sana) na yule Hua, Mungu, akitaka kuwaonyesha watu Wake upendo. Mungu anataka kupendwa. Mungu anataka kukupenda. “Mungu aliupenda ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na Uzima wa milele.” Bwana na abarikiwe! Basi Mungu, akitaka kuonyesha upendo, Yeye ilimbidi ninino... kufanya kitu kinachopendeka. Ilimbidi kufanya kitu kipole kama Yeye Mwenyewe. Ilimbidi kufanya kitu ambacho kingeweza kupendwa. Ilimbidi afanye kitu cha Asili Yake Mwenyewe.

³⁷ Hungeweza kupenda cho chote ambacho hakikuwa cha asili yako. Kupenda lazima kuungane na upendo. Mume na mke hawana budi kupendana, iwapo watafaulu. Jamaa haina budi kupendana, kama watafaulu. Kitu cha kupendwa! Utatafuta kila mahali, kumtafuta msichana awe mke wako ambaye unampenda. Yeye atatafuta, ampate mume ambaye angeweza kumpenda.

³⁸ Naye Mungu hutafuta, akijaribu kupata mtu ambaye Yeye anaweza kumpenda. Kwa hiyo, Yeye alijiwakilisha Mwenyewe hapa duniani kama Hua mpole na Mwana-Kondoo mpole. Kama huyo Mwana-Kondoo dakika moja angewahi kuchukua asili ya mbwa mwitu, anayetoa meno kwa ukali, Hua yule angeruka aende Zake mara moja, angejiendea zake.

³⁹ Bali mwa—mwa—mwana-kondoo, yeye hana akili nyingi. Mwana-kondoo ni kitu kimoja ambacho, kikipotea, kimepotea kabisa. Kondoo hawezi kujua njia ya kurudia. Hiyo ndiyo sababu mbuzi humwongoza mautini. Hawezi kujua njia, kondoo aliyepotea. Hiyo ndiyo sababu Mungu alitufananisha sisi na kondoo. Tukipotea, tumepotea. Hatuwezi kujitafuta. Na kuna njia moja tu ya kutenda jambo hilo, nayo ni, kujitua sisi wenyewe kwa Mchungaji wa kundi, Naye ataongoza.

⁴⁰ Sasa, ninapomwangalia huyu Mwana-Kondoo na kondoo pamoja... Mwana-Kondoo na Hua, hasa, pamoja, walifanyika mmoja. Ndipo angalia jinsi Hua alivyomwongoza Mwana-Kondoo, Mwana wa Mungu. Jinsi Yeye alivyokuwa mpole, akijua

kwamba Yeye anakwenda machinjioni. Jinsi Yeye alivyokuwa mpole, sikuzote kutojaribu kutenda Mwenyewe, kutojaribu kuwa ajitoshelezaye. Yeye alisema, “Sitendi neno mpaka Baba anionyeshe kwanza, na Baba anakaa ndani Yangu.”

⁴¹ Sasa, jambo jingine alivyo mwana-kondoo, mwana-kondoo yu tayari kuacha haki zake. Sasa, Mungu anataka sisi tuwe wana-kondoo, bali kuna wakati mwingi ambapo hatutaki kutoa haki zetu, kupoteza haki zetu. Wengi wenu husema, “Vema, nina haki, Ndugu Branham.” Hiyo ni kweli, lakini uko tayari kupoteza haki zako? Uko tayari kutoa haki zako, ili kwamba Mungu apate kukuongoza? Hiyo ndiyo shida ya makanisa yetu leo, mengi yao, kwamba upole wa Mwana-Kondoo wa Mungu . . . Tunapaswa kuwa wana-kondoo, tumekuwa kila kitu ila wana-kondoo. Na hiyo ndiyo sababu, mara tunaposhika msimamo huo, Hua wa Roho Mtakatifu anaruka anaenda Zake.

⁴² Kama Mwana-kondoo wa Mungu angeling’aka mara ya kwanza kama mbwa mwitu, au angefanya jambo lo lote kinyume cha yale Hua mpole angalivumilia, yule Hua angeliruka aende Zake. Angeliondoka mara moja.

⁴³ Na hiyo ndiyo sababu leo tunashangaa, “Hivi kanisa la Kipentekoste lina nini?” Ni kwa sababu tumechukua asili nyingine. Tumejitwalia asili ya kusema, “Tunataka haki zetu. Tutafanya yale tunayojua ni halali kufanya.” Nasi tumekuwa wenye kiburi. Tumekuwa wenye uhasama. Tumekuwa wasiojali. Tunaruhusu hasira ituingie. Tunaachia uchoyo utuingie.

⁴⁴ Mwana-kondoo, ifikapo wakati . . . Yeye anamiliki sufu yake mwenyewe, hizo ni haki zake. Sufu ni yake, bali humchukua mwana-kondoo na kumtupa juu ya ubao wa kunyolea, na kumfunga miguu. Yeye hapigi teke kamwe, hana fujo. Unamnyang’anya tu haki zake moja kwa moja, kwa sababu yeye ni mwana-kondoo. Hawezi kufanya kitu, kwa sababu hiyo ndiyo asili yake. Lakini siku moja muudhi Mkristo, utaona kama yeye ni mwana-kondoo au ni mbuzi. Utajua jinsi alivyo, ukimuudhi wakati mmoja. Na hiyo ndiyo sababu leo kwamba makanisa yetu yako katika hali yaliyo nayo.

⁴⁵ Tumejiita wana-kondoo wa Mungu. Wanawake kwa wanaume, pamoja, wameanza kutenda kila kitu na kuacha kuwa kama wana-kondoo wa Mungu. Waone wakitembea barabarani, wakiwa na nywele fupi, zilizokatwa, wamezirembesha nywele zao zote. Na miaka michache iliyopita, unaita . . . wewe, wao . . . usingewaajiri kufanya jambo hilo. Ndipo unashangaa ni kwa nini kanisa liko katika hali lililo nayo, ni kwa sababu umechukua asili ya mbwa mwitu au ya mbuzi, badala ya kukaa katika utiifu na unyenyekevu. Nanyi mnasema, “Hiyo ni haki yangu, Ndugu Branham.” Najua ni haki yako. “Vinyozi hukata nywele. Na maadamu kinyozi anakata nywele je, mimi sina haki?” Hilo ni kweli, hiyo ni haki yako ya Kimarekani. Bali

je, uko tayari kuitoa, kusudi uwe mwana-kondoo? Unakubali kujitoa?

⁴⁶ Nanyi wanawake, si muda mrefu uliopita, mngeshuka kwenda barabarani... Ni dhihaka kuona jinsi wanawake wanavyovalia leo. Nami sizungumzii kuhusu Mpresbiteri na Mmethodisti, ninazungumzia kuwahusu ninyi wanawake wa holiness. Mnashuka mnaenda barabarani, na ni . . .

⁴⁷ Nilikuwa na msalaba mdogo ulioning'inia mbele ya motokaa yangu, na mtu fulani akaniambia, kasema, "Billy, unajua hiyo ni alama ya Kikatoliki?"

⁴⁸ Nikasema, "Lini Wakatoliki walipata haki ya kutumia msalaba?" Hasha! Hiyo si alama ya imani ya Kikatoliki; hiyo ni alama ya imani ya Kikristo. Imani ya Kikatoliki ni maskini mtakatifu aliyekufa, ya Mariamu au—au mtu fulani aliyekufa ambaye wanamwabudu. Sisi hatuwaabudu watu waliokufa. Hatumwabudu Mtakatifu Cecelia na watakatifu hao wote mbalimbali. Huo ni Ukatoliki, ambao ni ibada ya hali ya juu ya mizimu. Bali msalaba unamwakilisha Yeye Ambaye alikufa na akafufuka tena.

⁴⁹ Nami nikasema, "Nauweka huo hapo, nikiangalia barabarani. Miaka ishirini na mitano iliyopita, au thelathini, nilipokuwa karibu kipofu, nilimwahidi Mungu iwapo Yeye angeyaponya macho yangu ningetazama jambo lililo halali." Kisha nikasema, "Kila mahali unapoangalia, ni uovu mwingi, wanawake nusu uchi, na wanawake walio uchi wamelala wiwanjani na kila mahali. Naangalia msalaba badala ya kuangalia, nakumbuka ambalo Kristo alinitendea, kisha nalipa kisogo jambo hilo . . . ambalo ni la Ibilisi." Haleluya!

⁵⁰ Na hapo, enyi watu, msiseme hao ni "Wapresbiteri, Wakatoliki," hao ni Wapentekoste! Amina. Unasema, "Ninayo haki, Ndugu Branham." Hilo ni kweli, bali kama ungekuwa mwana-kondoo, ungepoteza haki zako. Na unapotenda jinsi hiyo, Roho Mtakatifu, yule Hua mpole, anaruka akaenda Zake papo hapo. Hataaibishwa pamoja nawe. La, la. Usifikirie kamwe utatenda hivyo na bado ungali na Roho Mtakatifu. Huwezi kufanya hivyo! Biblia ilisema hivyo. Yakubidi upoteze haki . . . Vema, wasema, "Wanawake wengine wanalifanya."

⁵¹ Nanyi maskini wanaume wasio na mifupa, enyi madoandume, ninyi ambao mtawaruhusu wake zenu kufanya jambo kama hilo, hiyo yaonyesha ulichofanyizwa kwake. Hiyo ndiyo sababu huna Roho Mtakatifu kama unavyokiri kuwa Naye, la sivyo ungekuwa na kitu fulani cha kutosha kumfanya aenende kama bibi maadamu anaishi pamoja nawe, kwa vyo vyote. Amina. Hilo laonekana kama la kizamani, linakatakata. Bali hilo ndilo kanisa linahitaji leo, ni kuoshwa kwa mtindo wa kale, na Roho Mtakatifu, na kuanikwa nje lipate kukauka, na kupiga pasi, kwa Roho Mtakatifu. Hakika!

⁵² Hali gani ulimwengu umefikia! Jinsi wanavyojitokeza barabarani na kufanya yasiyofaa. Jinsi ambavyo unatokeza kichwa chako kwenye televisheni Jumatano usiku, na hutaenda kanisani! Jinsi ambavyo wewe, mbona, bali hakuna mtoto nchini. . . asiyejua habari zote za David Crockett. Na huo uongo mchafu, kusema eti aliva dubu akiwa na umri wa miaka mitatu, unajua huo ni uongo, bali unaruhusu watoto wako wajaze vichwa vyao na upuzi kama huo. Na hakuna asilimia moja toka kwa mia moja ambayo imewahi kujua cho chote kuhusu Yesu Kristo. Ni kwa sababu ulimwengu huu umechafuliwa sana! Taifa hili, ni la kipuzi sana na liko mbali sana na Mungu, limemkataa Roho Mtakatifu.

⁵³ Loo, unasema, “Ninakwenda kanisani na kupaza sauti.” Waweza ukafanye hivyo. Bali, mpaka huyo Mwana-kondoo wa Mungu mpole atakapotulia moyoni mwako, na akufanye usafishe maisha yako na kutenda kama mtu tofauti, haitakufaidia kitu kuigiza Ukristo. Yakubidi uwe nao. Amina.

⁵⁴ Nilikwenda kwenye nyumba moja hapa si muda mrefu uliopita, kumwona mgonjwa, na bibi fulani alikuwa amelala, ameketi pale. Na maskini Oswald akaingia, amevaa kofia upande, akasema, “Mama, chakula cha kutwa tayari?”

⁵⁵ Akasema, “Mpenzi, hatujapata nafasi” kasema, “asubuhi hii kupika chakula cha mchana.” Akasema, “Ninakutengenezea sambusa,” akasema, “kuna machungwa machache.”

⁵⁶ Aliondoka akaokota chungwa, akaliangalia, akaling’ata, akalitupa kwenye ukuta kwa nguvu sana alivyoweza, maji yakachuruzika, akasema, “Kama ni hicho tu mlichu nacho hapa, basi nitatoka niende zangu,” namna hiyo.

⁵⁷ Nikawaza, “Ee Mungu, laiti angelikuwa wangu kwa yapata dakika tano!” Aisee, ningemchuna ngozi namna asivyowahi kujua huchunwa! Bali wao waliketi pale, wanasikitika na kubembeleza. Analohitaji ni mtindo mzuri wa kale wa kumtandika vizuri. Hilo ndilo tunahitaji, nyumba za mitindo ya kale tena, na baadhi ya wahubiri ambao watasimama nyuma ya mimbara na kuhubiri Ukweli, na kuliweka Hilo mahali linapopaswa kuwa. Amina. Hiyo ni kweli. Loo, jamani!

⁵⁸ Maskini Mariamu mdogo anatarisha miguu yake na kuinua pua lake dogo juu na kubinua midomo yake yenye rangi nyekundu (ya vipodozi vya Max Factor) juu, na kuinua kichwa chake kidogo juu na kutoka nyumbani. Ni fedheha jinsi gani! Jinsi watoto wanaendelea kuwa wasiotii! Biblia ilisema wangekuwa hivyo. Maandiko yalisema wangekuwa hivyo. Vile wangentenda, vile wangepanya, na mambo yanayotendeka ulimwenguni leo, ni kwa sababu wamemhuzunisha Roho Mtakatifu hata akaondoka.

⁵⁹ Miaka michache iliyopita. Nitasherehekea sasa mnamo siku chache zijazo kushuka mara ya kwanza kwa Roho

Mtakatifu Marekani, miaka hamsini iliyopita mwaka huu, kwenye mkutano ule wa zamani kwenye Barabara ya Azusa, mkutano wa kipentekoste huko Los Angeles, ambako wao walishukiwa na Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza, wakati watu walipokusanyika pamoja. Wakati Kristo aliposhuka miongoni mwa watu hao, walikuwa wapole tu, wenye amani tu. Waliishi maisha ya kitauwa. Waliishi maisha ya kujitolea. Walikuwa wako tayari kujitoa. Walikuwa tayari kuongozwa na Roho Mtakatifu. Hawakujali walichosema watu, walikuwa wa “mtindo wa kikale,” kama walisema walikuwa “wenda wazimu” au cho chote kile, walikuwa tayari kuongozwa na Roho Mtakatifu.

⁶⁰ Bali, leo, loo, jamani, wakiwa na kibonge cha kupakalia poda na jaluba la vipodozi, na wamevaa kaptura, wakaenda barabarani, mbona, ni aibu! Na kujiita wenyewe, “wenye Roho Mtakatifu.” Loo, unasema, “Lakini nilinena kwa lugha.” Ndiyo, Ibilisi hunena, pia. “Loo, nilipaza sauti kwa nguvu.” Na ibilisi hunena, pia. Ibilisi anaweza kuigiza kila kitu alichu nacho Mungu, isipokuwa upendo, na yeye hawezi kuigiza upendo. Ndiyo.

⁶¹ Basi, punde si punde, ulipoanza kufanya mambo hayo, ulifungua mlango, ukaanza kupatana, ndipo kanisa likaanza kupata milio midogo ya kuku, vikundi vidogo-vidogo miongoni mwao, na huyu mmoja akasema, “Unajua, mchungaji yuko tu *hivi na vile*,” au “shemasi yuko *kadha na kadha*.” Na, jambo la kwanza wajua, ukasikiliza hilo! Na hiyo ndiyo sababu mna matatizo mengi, ni kwa sababu mlianza kumsikiliza Ibilisi, mkapata mng’ako badala ya kumsikiliza Hua mpole, Roho Mtakatifu, Hua wa Mungu ambaye angewaongozeni na kuwaonyesheni njia, na kuwapenda na kuwabariki.

⁶² Mara ya kwanza unapata hivyo vipindi vidogo-vidogo vya hasira kali, Hua anaruka mara moja. Hiyo ni kweli. Hawezi kuvumilia. Asili yake ni tofauti. Loo, Yeye hawezi kuvumilia jambo hilo hata kidogo. Na unapoanza kuzungumza mambo ya jirani yako, hawezi kuvumilia jambo hilo, Yeye hatachukuana nalo. Hujirukia tu na kwenda Zake. Hawezi kulivumilia zaidi. Hua ni mpole. Hua ni mtiifu, na Hua, na—na hawezi kuvumilia kitu kingine isipokuwa kiwe cha asili ile ile.

⁶³ Sasa, Mungu anaweza kukufanya uwe na asili nyingine, mwanamume au mwanamke, Yeye anaweza akupe asili nyingine. Basi unasema, “Vema, Ndugu Branham, tutendeje kuhusu jambo hilo?” Wewe uwe tu mwana-kondoo tena. Ni wanyama wawili tu watakaoshirikiana pamoja, hao ni hua na mwana-kondoo. Hua hatakiia kitu cho chote isipokuwa mwana-kondoo. Na kama umekuwa mbuzi, basi ondoa ile roho ya kale ya mbuzi kwako. Hiyo ni kweli. Kama umekuwa kitu kingine, kiondoshe kwako, kama umeanza kuwa mpayukaji.

64 Hapa wakati mmoja, nilihubiri kwa nguvu nilivyoweza kuhubiri katika mji fulani, na palikuwapo na maelfu ya watu pale. Nikatoa wito wa madhabahuni. Nilidhani ningegusia kila namna ya dhambi, niligusia kila kitu ambacho niliweza kukifikiria. Usiku ule baada ya ibada kwisha, maskini mwanamke kimbelebele alisogea karibu, akasema, “Vema, Ndugu Branham, ninafurahi kwa kweli hukunigusa mimi usiku wa leo.”

Nikafikiri, “Huyo lazima awe Mkristo hasa.”

Kasema, “Hukunigusa usiku wa leo.”

65 Nikasema, “Vema, kwa hakika nina furaha kusikia hivyo, bibi, bila shaka u karibu na Ufalme wa Mungu.” Na akainama akaondoka.

66 Bibi mzee amesimama pale. Nikasema, “Ati, unamjua mwanamke yule?”

“Ndiyo.”

Nikasema, “Bila shaka ni Mkristo hasa.”

67 Kasema, “Ulishindwa kukemea jambo moja usiku wa leo, Ndugu Branham, nalo ni kusengenyanana. Yeye ndiye msengenyanaji hodari sana nchini.” Basi, ndivyo ilivyo, unaona.

68 Bali unapofikia mojawapo ya mambo hayo, haidhuru kama mhubiri anayekemea mimbarani au la, unapoona mambo hayo ya kimwili ya ulimwengu, maadamu mnayavumilia, mko mbali na Mungu, na Roho Mtakatifu ataondoka. Hiyo ndiyo sababu mikutano haiko vile ilivyokuwa. Hiyo ndiyo sababu mburuzo wa vumbi la mbao hauonekani asubuhi hii katika Maskani. Hiyo ndiyo sababu mikutano mikuu ya hema haipo nchini, ni kwa sababu tumemhuzunisha Hua mpole wa Mungu. Hiyo ni kweli. Yeye hatakaa nasi maadamu tu watu wasiojali namna hii, maadamu sisi ni wasengenyanaji, “Tunataka kufanya tupendavyo.”

69 Sasa, nataka uangalie, yule mwana-kondoo alikuwa mwana-kondoo mnyamavu. Biblia ilisema, “Yeye hakufungua kinywa Chake. Kama kondoo anyamazavyo mbele yao wakatao manyoya yake, Yeye alikuwa kimya.” Hakufungua kinywa Chake. Yeye hakuwa jamaa anayetaka haki zake. La, bwana, Yeye alikuwa tayari kupoteza haki Zake. Alikuwa Mwana-Kondoo mnyamavu.

70 Bali, leo, loo, jamani, jinsi tunavyotaka tofauti zetu! Loo, jamani! “Nakwambia, hebu acha mtu aninenee jambo fulani, nitaondoka niende nikamshike, nakwambia, nitamharibu. Huyo mwanamke mnafiki atanijuta nitakapomwona! Ngojea tu mpaka nimpate! Mungu na abarikiwe, haleluya! M-hu!” Hua anaruka tu akaenda Zake. Hiyo ni kweli. Roho Mtakatifu hayupo pamoja nawe tena, maadamu unajisikia jinsi hiyo. Hebu liandike tu hilo kwenye kitabu chako, Yeye hatatenda hivyo. Roho

Mtakatifu hatakaa ambapo pana roho ya namna hiyo. Inabidi iwe roho ya mwana-kondoo, roho pole, au Yeye hatakaa nayo, ni hayo tu; kama si pole, tiifu, iongozwayo na Roho Mtakatifu. Na kama lo lote likitukia, hata Yeye halioni, anaendelea tu. Unaona? Mara tu hiyo iachapo njia, unajua, hapo ndipo hasa. . . ulipoacha njia.

⁷¹ Unajua, dhambi ya kwanza ilianza kwa mtu kuacha njia kidogo tu. Ulijua hivyo? Biblia ilisema hivyo. Hawa aliacha njia kidogo tu, kusikiliza maneno ya Shetani, ndipo akamchorea picha nzuri sana mpaka kwa kweli akafikiri ilikuwa ni Kweli. Basi akamsikiliza.

⁷² Na jambo pekee Ibilisi analotaka wewe ufanye, ni kuacha njia kidogo tu kwa dakika chache. Anaweza kuchora picha, akasema, “Sasa, hebu angalia hapa. Unajua, ndugu, unajua, dada, kama wangekuwa watu wazuri, wasingalitenda *hili*. Kama walitenda *hili* papa hapa, unajua.” Anaweza kulifanya liwe la kweli kwako mpaka linakuwa ukweli hasa. Naam! Bali kumbuka, ni Ibilisi.

⁷³ Mimi sijali wao wameshuka kiasi gani, kiasi gani wamezama katika dhambi, ni wajibu wako kuwakumbatia na kuwainua kwa upendo wa Mungu. Ulikuwa wapi wakati Hua wa Mungu alipokuinua kutoka kwenye matope ya udongo wa mfinyanzi? Ni wajibu wako, rafiki yangu. Ulimwengu huu unakufa kwa njaa ya upendo kidogo. Ile. . .

⁷⁴ Nataka umwangelie mnyama huyu, pia, mnyama huyu mdogo, alikuwa mwana-kondoo mnyamavu kwa sababu haku. . . Yeye aliposhutumiwa, Yeye hakushutumu. Hakushutumu na kufanya yasiyofaa, na fujo na kufoka maneno na kadhalika, Yeye hakulifanya hilo. Mtu fulani. . . Wakati Yeye aliposhutumiwa, hakushutumu. Yeye hakufungua kinywa Chake.

⁷⁵ Bali hebu acha mtu fulani akutende wewe au mimi jambo fulani, loo, jamani, tunalipuka kama chura aliyelipuliwa kwa risasi kubwa, tunafura kama—kama bata bukini mzee. “Nakwambia sasa hivi, akiniudhi hivyo tena, sitarudi kamwe kwenye kanisa hilo kuukuu tena. La, bwana! Mungu na abarikiwe! Haleluya! Wanazarayo watanipokea, Wapilgrim Holiness, watanichukua. Haleluya. Hainilazimu kufanya hivyo tena.” Vema, Hua anaruka anaenda Zake.

⁷⁶ “Wajua nini? Kama maskini mnafikiri huyo atahudhuria kanisa lile, sitakwenda huko tena. Mungu na abarikiwe, sitakwenda kamwe!” Kitu hicho kinapokupata, yule mbwa mwitu wa kale ang’akaye, Hua anaruka anaenda Zake. Kweli. Ndipo basi Roho Mtakatifu ameondoka.

⁷⁷ Ndipo mnashangaa mna nini. Mnashangaa kanisa lina nini. Mnashangaa mna nini. Kwa nini huna ushindi kama uliokuwa

nao? Umehadili asili yako. Umekuwa mbuzi badala ya mwana-kondoo. Umekuwa kitu kingine mbali na mwana-kondoo.

⁷⁸ Yakubidi umpate yule Roho mpole hasa. “Roho Mtakatifu na aniongoze po pote. Mungu, nampenda kila mwenye dhambi, haidhuru wako wapi.” Mahali pa namna hiyo pakiingia katika moyo wa mwanadamu, basi utaona kitu fulani kikitukia, nafsi yako.

⁷⁹ Unasema, “Vema, Ndugu Branham, je, kuna suluhisho lo lote kwa jambo hilo?” Ndiyo, kuwa tu mwana-kondoo, hilo tu. Unasema, “Vema, Ndugu Branham!”

⁸⁰ Nilikutana na kijana mwanamke hivi majuzi usiku, huko Shreveport. Mimi na Billy tulikwenda mahali fulani kununua sambusa baada ya ibada kumalizika. Kijana mwanamke mrembo akaingia mle ndani, pengine ni msichana mdogo, au labda umri wa miaka ishirini au kitu kama hicho, amevalia vizuri. Akaketi chini. Niliona kwamba alishikilia kuangalia upande ule. Mimi niliendelea tu kula. Dakika chache yule bibi akaingia. Akasema, “U hali gani?” Nikazungumza naye. Nami najua huyo bibi alikuwa ni Dada Davis kule. Na yeye na bibi mwingine kutoka Maskani ya Uzima, niliwajua vizuri, akaja akazungumza nami, akaendelea. Kisha yule msichana aliyeketi upande mwingine, akasema, “Ndugu Branham, huo ulikuwa Ujumbe mzuri usiku wa leo.”

⁸¹ Nikasema, “U hali gani, dada?” Nikasema, “Asante, sana.” Kisha nikasema, “Wewe ni mshiriki wa Maskani ya Uzima?”

⁸² Akasema, “Ndiyo.” Akasema, “Unajua, Ndugu Branham, ningeweza kuimba kwenye kwaya, lakini wanatoa masharti huko.” Akasema, “Nilipata, loo, miaka mingi ya mafunzo ya sauti, na kila kitu.” Akasema, “Niliimba nyimbo za mtu mmoja-mmoja na naliimba mambo fulani.” Akasema, “Bali, si-sikuweza kuimba, kwa sababu wana-wana masharti kwamba ‘hakuna mwanamke aliyepodoa anaweza kuimba-kuimba katika kwaya.’”

Nikasema, “Naam, Mungu asifiwe kwa Maskani ya Uzima!”

⁸³ Akasema, “Vema, nakuambia, Ndugu Branham,” akasema, “mimi ni Mkristo.”

⁸⁴ Nikasema, “Basi, dada, nenda nyumbani ukanawe uso wako au cho chote ufanyacho.” Nikasema, “Unataka kuniambia kwamba ungeruhusu jambo dogo kama kujipaka kidogo takataka hiyo usoni mwako. . . .”

⁸⁵ Nami naweza kukuthibishia kwamba hilo lilitokana na Ibilisi. Naweza kukuthibitishia kwamba hakuna cho chote katika . . . Waanzilishi wake ni makafiri. Na maadamu unajipaka hiyo, ni alama ya ukafiri. Sasa, hivi karibuni nimerudi kutoka Afrika, na nimekuweko kwenye misitu ya Wahotentoti na kuona kabisa ambapo pete za masikio, ambako takataka

yote hiyo ilitoka, na zote hizi, johari nyingi zilizozungushiwa shingoni mwenu na masikioni na kila kitu, ambako hizo zilitoka. Ni makafiri. Na Biblia haitaki Mkristo awe kafiri. Na wewe hutaki. . . Sisemi kwamba wewe u mkafiri kwa sababu unalitenda, bali unajifanya ufanane na mmoja wao. Ni kwa sababu mchungaji wako hakukwambia Ukweli. Biblia ilisema hivyo.

⁸⁶ Na sasa unasema, “Ndugu Branham, nafikiri kama nina nywele fupi, inaniburudisha na kitu kama hicho.” Hilo ni kweli, lakini kama ungalikuwa na nywele ndefu ungeburudika zaidi. Ingeondoka yote shingoni mwako, nawe uisokote na kuiweka sawa.

⁸⁷ Mbona, unajua Biblia ilisema nini? Kwamba, mwanamume anayo haki ya kumwacha mkewe na kumtaliki kama akikata nywele zake. Kama akikata nywele zake, inaonyesha si mwaminifu kwake. Biblia ilisema hivyo, I Wakorintho 12, chunguza kama Hilo si kweli. Yeye ambaye. . . Mwanamke ambaye hukata nywele zake yuaaibisha kichwa chake, ambacho ni mume wake. Na kama yeye anamwaibisha, anapaswa atalikiwe na kuachwa. Hiyo ni kweli. Bali, unaona, mchungaji hakuambii kamwe mambo hayo. Na hiyo ndiyo sababu unatenda jinsi unavyotenda. Na—na yule mume, Biblia ilisema. . .

⁸⁸ Hapa si muda mrefu uliopita kuna mtu aliyeniandikia akasema, “Ndugu Branham, hizi—hizi blauzi ambazo wananunua wanawake,” akasema, “mbona, imekuwa kwamba ni. . . ni shida sana kupata blauzi tena, basi ni vyema kwa sisi wanawake Wakristo kuvaa hizi dakroni, nailoni, au cho chote kile?”

⁸⁹ Nikasema, “Angalia, dada, kuna jambo moja kwake. Hapa pana jambo moja ambalo ni kweli. Waweza kufanya hivi: kama huwezi kununua moja, wanauza cherehani, unaweza kushona moja.” Nikasema, “Hiyo ni kweli. Kuifanya ionekane tu. . .” Naamini, unajua, kilicho moyoni mwako ndicho kinachojidhihirisha chenyewe. Jinsi unavyotenda na jinsi unavyonena, hilo huonyesha kilicho ndani yako.

⁹⁰ Hiyo ndiyo sababu kwamba huku kung’aka kote hapa na kugombana na kusengenyana, na—na kuumana, na kufanya yasiyofaa kanisani, jambo hilo ndilo linalovunja kanisa. Hilo laonyesha kwamba Ibilisi amewapagaa, na hiyo ni kuonyesha Roho Mtakatifu amewaacha. Sasa, najua huko ni kuwaumiza tu baadhi yenu, lakini inapaswa kufanya hivyo. Inapaswa! Hiyo ndiyo sababu linanenwa; siyo kuwa mjanja, si kujifanya mwerevu; bali kuwaambieni palipo na matatizo, kwa maana siku moja itanibidi kusimama hukumuni kutoa hesabu kwa ajili yenu. Na sababu yenyewe hasa ya kutenda unavyotenda na kuenenda unavyoenenda, hiyo yaonyesha ulivyo. Iwapo una hasira ya kale ambayo italipuka bila breki wakati mdogo tu, na

kutoka hapa na kufanya yasiyofaaa, na kulaumu, au ukosefu wa adabu na upuzi kama huo, hiyo yaonyesha inakotoka.

⁹¹ Sasa kuna jambo moja tu la kufanya, ondoa jambo hilo humo, ndipo Hua atarudi moyoni mwako. Wakati hua alipotoka kwenye safina, aliachiliwa. Lakini alirudi akapiga hodi kwenye mlango wenye giza hadi Nuhu alipomruhusu aingie ndani. Roho Mtakatifu yupo hapa. Roho Mtakatifu anataka kuingia. Hiyo ndiyo sababu leo, kwamba Roho Mtakatifu, Yeye hajakuacha kabisa. Ameketi tu nje kule kwenye matawi ya miti mahali fulani, yuko tayari kuruka arudi aingie ndani yako, akupe upendo na amani na furaha kama uliyozoea kuwa nayo. Hakika, Yuko tayari. Yuko tayari kutenda jambo hilo. Yeye anataka kutenda hilo. Yeye anatamani kutenda hilo. Bali wewe hutamruhusu Yeye afanye hivyo.

⁹² Sasa, mimi sizungumzi na ninyi wageni. Sijui ambalo mchungaji wenu. . . Ninazungumza na Maskani ya Branham. Sizungumzi na ninyi watu toka makanisa mengine. Ninazungumza na Maskani ya Branham. Hiyo ndiyo shida iliyopo mahali hapa.

⁹³ Hicho ndicho kinachomfanya Hua aruke aende Zake. Hebu mtu fulani aanzishe kitu kidogo kanisani, na jambo la kwanza, “Loo, hivyo ndivyo ilivyo? Loo, eti nini? Humaanishi hivyo?” Papo hapo Roho Mtakatifu anaondoka, anaruka anaenda zake. Yeye hawezi kuvumilia roho ya namna hiyo. Maadamu tabia hiyo ya mwana-kondoo inakutoka, basi Roho Mtakatifu ameondoka. Hiyo ni kweli. Na hiyo ndiyo shida leo hii. Hiyo ndiyo sababu watu wako katika hali waliyo nayo, ni kwa sababu wameachilia roho mbaya aingie mioyoni mwao, katika maisha yao. Sasa hiyo ndiyo sababu tuna. . .

⁹⁴ Biblia ilisema hiyo ndiyo sababu wapo wagonjwa wengi sana na wanaoteseka miongoni mwenu, ni kwa sababu ya mambo kama hayo. Twapaswa tuwe wapole. Twapaswa tujae amani. Lazima tuwe wanakondoo, ili Hua akae pamoja nasi.

⁹⁵ Sasa, kumbuka, Hua atakuja. Ulisema, “Loo. Ndugu Branham, usiniambie sijampokea kamwe Roho Mtakatifu. Haleluya! Kule, ule usiku kule siku moja usiku, loo, Yeye alipoingia ndani, niliweza tu kutembea. . .” Mbona, huyo alikuwa ni Yeye! “Loo, nilijisikia vizuri sana, nilijisikia kama ningeweza kumshika kila ndege mdogo mtini na kumkumbatia na kumpenda. Mtu ambaye ni mwovu kuliko wote kwangu aliyewahi kutenda kitu cho chote kwangu, nilijisikia kama ningeweza kumshika kwa mikono yangu na kumkumbatia. Loo, Ndugu Branham, jinsi nilivyojisikia!” Hakika, huyo alikuwa ni Roho Mtakatifu.

⁹⁶ Bali, unaona, sababu Yeye hakuweza kukaa. Wakati huo wewe ulikuwa mwana-kondoo; bali ulipofanyika mbwa mwitu, ilimbidi Yeye aruke aende Zake. Hakuna kosa kwa yule—

kwa yule—yule Hua; ni wewe, nawe. . . uliporuhusu roho yule aje kwako. “Hivi nimenaruhusu, Ndugu Branham?” Ndiyo, ulipoanza kusikiza yale masengenyo, uliposikiliza uongo ule, ulipoanza kusema, “Vema, nina haki ya kufanya hivyo!”

⁹⁷ Huna haki yo yote. Umenunuliwa kwa thamani, hiyo ilikuwa gharama ya Damu ya thamani ya Mwana wa Mungu. Huna haki halali. Haleluya! Haki pekee ulizo nazo, ni, kuja kwenye Chemchemi iliyojawa na Damu itokayo kwenye Vena ya Imanueli, wakati wenye dhambi wanapozamishwa kwenye gharika hiyo husafiwa taka zao zote za hatia. Ndiyo, bwana. Hizo ndizo haki pekee ulizo nazo, ni kujitolea kwa hiari yako, kwa Mungu, ndipo Mungu anakuongoza tangu wakati huo. Hiyo ndiyo inasababisha mikutano. . . Hiyo ndiyo inayosababisha mambo mengi sana ya ajabu. Roho Mtakatifu ataenda mahali, Roho Mtakatifu alisema, “Hili si sahihi. Simamisha mkutano, ondoka uende kule.” Nitausimamisha, pia, ndugu, endelea mbele. Hiyo ni kweli, kwa sababu yakubidi uongozwe na Roho wa Mungu Na njia pekee ya kuongozwa na Roho wa Mungu, ni kuwa mpole, si kujua mengi.

⁹⁸ Loo, unafikiri, “Najua mengi.” Ndiyo, unaifanya akili yako ifikiri sana na haiwezi hata kufanya kazi. Wewe unajua vitabu vyote na majibu yote, na Kiyunani chote na Kiebrania chote, na huna mahali pa kupumzikia Hua. Hiyo ni kweli. Bali unajua mambo yote, basi Hua hawezi kuongoza, sababu unajua mengi kupita kiasi.

⁹⁹ Mwana-kondoo hadai kujua cho chote. Apaswa awe na mtu mwingine wa kumwongoza. Utukufu! Basi. Hujui kitu! Amina. Jambo pekee nijualo, ni, Kristo Yesu alikufa apate kuniokoa.

¹⁰⁰ Mtu mmoja alipitia kule California, alikuwa na maandishi mbele yake, yakasema, “Mimi ni mpumbavu wa Kristo,” na huko nyuma kasema, “Wewe u mpumbavu wa nani?” Hiyo ni kweli. Uwe mpumbavu, kwa ulimwengu, ili uweze kuongozwa na Roho Mtakatifu, maana wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho Mtakatifu. Warumi 8:1, kasema, “Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kufuata mambo ya mwili, bali mambo ya Roho,” wasioenda kwa kufuata mambo ya mbwa mwitu, bali Hua. Amina.

¹⁰¹ Doc alipendelea kuimba wimbo, “Jaza mapito yangu kila siku kwa upendo, nitembeapo na Hua wa Mbinguni; nijalie kutembea wakati wote nikiimba na kutabasamu, jaza mapito yangu kila siku kwa upendo.” Itakuwa siku ya amani jinsi gani kwa Maskani ya Branham, au kanisa lingine lo lote au mtu ye yote binafsi, watakapoachilia haki zao, wapate kuwa mwana-kondoo.

“Swala ni nini, Ndugu Branham?”

102 Rudi uwe mwana-kondoo, rudi uwe mpole, rudi kwenye kuwa mtu asiyejua kitu, rudi kwenye kujitoa mwenyewe kwa Kristo. Usijaribu, usijaribu kujua kitu. Enenda kwa uvumilivu, utaratibu, unyenyekevu, utulivu, naye Hua atakuongoza. Lakini kila unapoona . . . unapoanza kusikiliza masengenyo hayo, kila unapoanza kupandisha hasira ile, kila unapoanza kufikiria kwamba una haki ya kufanya *hili* na kufanya *lile*, Hua anaruka anaenda Zake. Ndipo huna Huyo tena. Sasa, hayupo mbali sana nawe asubuhi hii, enyi kanisa. Ameketi nje huko kwenye tawi la amani, akingojea tabia yako ibadilishwe. Amina.

103 Unachohitaji leo ni kusalimisha haki zako zote, ni kumwacha Mungu akulaze chini na kukunyoa haki zako zote aziondoe kwako. Amina. Unaweza kufikiria jinsi mwana-kondoo mdogo, yote—sufu yote ikining'inia juu yake? Hiyo ni haki yake, ndiyo. [Ndugu Branham anaigiza mwana-kondoo anayehema—Mh.], akiona joto, na kisha alale tu juu ya meza ya kukatia sufu. Wanajua kinachomfaa. Wanaoondoa haki zake zote kwake na kuzikata zote, jinsi akimbiavyo ameburudika na ni mwepesi. Jamani, jamani, ana furaha, ana furaha, na anarukia huku na huko na ana furaha sana. Ndiyo, bwana. Kama utapoteza haki zako, hilo ndilo unalopata. Bali yakubidi kupoteza haki zako na kuachilia Neno la Mungu likate ulimwengu wote liutoe kwako, likuondolee mbali tabia zote za ulimwengu, upate kuwa kiumbe kipya katika Kristo.

104 Hapa hivi majuzi, huko Afrika, nilikuwa nikizingumza na—na mzee fulani mtakatifu. Akasema, “Ndugu Branham, najua unaamini mambo ya kimbinguni.”

Nikasema, “Bila shaka, ndugu yangu.”

105 Akasema, “Miaka mingi iliyopita nilikuwa nikifikiria nilikuwa mtu mashuhuri.” Akasema, “Nilifikiria nilikuwa Mkristo hasa.” Kisha akasema, “Basi huko kanisani mwetu . . . Ilinibidi nikwee kilima, mahali niliposimamisha gari langu dogo.” Akasema, “Ilinibidi nipande kilima kama, loo, yadi mia tatu au mia nne, na kupita vichakani, na kadhalika, kupanda.” Akasema, “Tulifanya mkutano wa maombi juu kule.” Ndipo akasema, “Nilifikiri mimi nilikuwa Mkristo kwelikweli.” Akasema, “Nilijua Biblia yote. Nilijifunza Kiebrania chote. Nilijifunza matamshi yote sahihi ya neno.” Akasema, “Kama mtu ye yote angenikaribia, ningeweza” [Ndugu Branham anadata kidole chake—Mh.] “kuzungumza nao hivyo kuhusu Biblia. Nilijua ambacho nilikuwa ninakizungumzia.” Akasema, “Usiku mmoja nilikuwa ninakwenda kanisani. Kumekuweko na mizozo mingi kanisani mwetu.” Akasema, “Kulikuwa na vikundi vidogo-vidogo vinavyozozana. Unajua jinsi vinavyoanza.”

Nikasema, “Ndiyo, bwana.”

106 Akasema, “Nilipokuwa nikipanda kile kilima, nilikuwa ninatembea, mara moja nikahisi kwamba kuna mtu

anayenifuata.” Akasema, “Nikawaza ningengojea tu kidogo kwa ye yote yule, aje anifikie, na ningezungumza nao kwa muda kidogo wakati tunapanda barabarani.” Unajua, hilo ni jambo zuri, unangojea tu muda kidogo. Kisha akasema, “Nilipokuwa ninapanda juu kilimani,” kasema, “nikapanda juu. Mtu fulani akapanda akaja kule kilimani,” akasema, “Yeye alikuwa na robota mgongoni Mwake ambalo lilikuwa kubwa kuliko yule Mtu.” Basi akasema, “Yeye alikuwa anahema tu na kutoa pumzi kwa nguvu, huku anapiga hatua ndogo fupi-fupi, akijaribu kupanda. Nami nikasema, ‘Ewe jamaa, wataka nikusaidie kuubeba mzigo huu kuupeleka juu kilimani?’ Akasema, ‘La, yanipasa niubebe.’” Kasema, “Nikatazama mkono Wake,” kasema, “Hapo nikajua lilikuwa ni ono. Alikuwa na makovu mikononi Mwake.” Kasema, “Nilianguka chini, nikasema, ‘Bwana, Wewe unabeba dhambi za ulimwengu katika gunia hilo?’ Yeye akasema, ‘La, ninabeba zako tu. Kukukweza kilimani, ili kwamba uweze tu kupanda.’”

¹⁰⁷ Hivyo ndivyo ilivyo. Kama tungeangalia huku na huko, tungeona kwamba Yeye anabeba zetu. Je, hilo haliwafanyi mjisikie watu duni? Mioyo yetu miovu, mikatili, eti tu kwa sababu tunaweza kufanya jambo hilo.

¹⁰⁸ Hapa wakati fulani uliopita nilikuwa ninawinda. Kama mjuavyo, napenda kuwinda. Na kulikuwa na mtu mkatili katika mkoa ule, alikuwa mtu mkatili. Naye alipendelea kunifanyia mzaha kwa sababu singepiga risasi kulungu jike na watoto wake. Nilisema, “Ni ukatili.” Nikasema, “Kwa nini usiwe mwindaji mzuri hasa, uwaue kulungu wazee na kadhalika ambao ni wazee na wako karibu kufa. Mungu alitupa sisi hao, na uwaache hao mama wadogo na kadhalika.”

¹⁰⁹ Akasema, “Aha, mhubiri, mwenye moyo wa kuku wee!” Akaendelea kuniambia namna hiyo.

¹¹⁰ Nikasema, “Sasa, angalia, kama nina njaa na ninataka mmoja wa hao watoto wa kulungu, naamini Mungu angeniruhusu niwapate. Lakini kumuua tu kusudi nionekane hodari,” naam, angejaza gari nzima. Naye alikwenda akajitengenezea kitu cha kuitia, namna fulani ya filimbi, naye aliweza kuipuliza ile filimbi ikasikika sawa kabisa na mtoto wa kulungu anayeita. Siku moja tulikuwa huko msituni pamoja. Nilimwaibisha, nikasema, “Ningeona aibu mimi.” Aliuwa watoto wanane au kumi wa kulungu wakati mmoja, kama angaliweza, kulungu jike na kila kitu, ati aonekane tu ni hodari, pengine akate miguu ya nyuma na kuacha sehemu iliyobakia pale. Nikasema, “Haikupasi kufanya hivyo.”

“Aha,” akasema, “ninyi wahubiri ni waoga mno!”

¹¹¹ Siku moja alisimama nyuma kwenye vichaka, alikuwa ameshika hii filimbi na kuipiga, basi ikalia kama mtoto wa kulungu anayelia. Mara tu alipofanya hivyo, kulungu

jike anayependeza akatokeza kichwa chake, akaja akichapua miguu. Ungeweza kuona macho yake makubwa ya kahawia yakiangalia. Alikuwa ameshtuka. Alikuwa anatazama hapa na pale. Mwindaji yule akainuka, akalenga bunduki yake ampige yule kulungu jike. Basi yule kulungu akamwona yule mwindaji. Lakini, unajua nini, mlio ule wa yule mtoto, hakuona bunduki ile. Alikuwa anamtafuta yule mtoto, alikuwa katika shida. Unajua, hilo ni onyesha halisi la umama na upendo wa mama, kwamba angekabili bunduki ile usoni, kwa mauti, akiangalia hayo kwenye mtutu wa bunduki ile. Unajua nini, onyesho lile lilikuwa kubwa sana, lilimwingia, akatupa chini bunduki yake! Akarudi mbio akanishika ghafla mkononi, akasema, “Billy, niombe, nimetosheka na jambo hili!” Alipoona lile onyesho la ushujaa wa mama!

¹¹² Loo, ulimwengu unapona onyesho la upendo wa Mungu, na ushujaa katika mioyo yetu ya kibinadamu, itakuwa tofauti namna gani. Tunapomruhusu Hua wa Mungu aje mioyoni mwetu na kutufanya wapole, kutufanya wavumilivu.

¹¹³ Huko katika kivuli cha vichaka nyuma kule, mimi nikisimama kule nikimwombea maskini jamaa yule, nilimwongoza kwa Bwana Yesu. Tangu wakati huo, alikuwa mwindaji mzuri na asiye na lawama.

¹¹⁴ Hakika, alifikiria alikuwa na haki, angetenda atakalo. “Wao wako kwangu, wanakula majani ya ng’ombe chini huko wakitaka.”

¹¹⁵ Nikasema, “Hiyo ni kweli, lakini kutenda hivyo si utu.” Yakubidi upoteze haki zako. Ee, Mungu turehemu, tupate kupoteza haki zetu.

¹¹⁶ Hapa wakati fulani uliopita, mnamo, loo, kama miaka mia moja iliyopita, kulikuwa na Mkristo maarufu aliyeishi Marekani ya kusini-magharibi. Jina lake lilikuwa Danieli Curry, mtu mzuri sana, mcha Mungu, mtauwa, Mkristo kwelikweli, mtu ambaye alipendwa na kila mtu, mtu mzuri sana. Na hadithi inaelezea, kwamba alikufa au akalala usingizi mzito sana, naye alisema . . . alipokuwa anakwenda Mbinguni, bila shaka, wakati alipokufa. Na wakati alipofikia yale malango ya lulu, bawabu alikuja mlangoni, akasema, “Wewe ni nani?”

¹¹⁷ Akasema, “Mimi ni yule mwinjilisti, Daniel Curry, nimevuta maelfu ya watu kwa Kristo. Nami ni . . . Nataka kuingia humo ndani asubuhi ya leo. Safari yangu ya maisha duniani imekwisha, sina mahali pa kwenda sasa.”

¹¹⁸ Hayo ndiyo yatakayokupata asubuhi moja, ewe mwenye dhambi. Hayo ndiyo yatakayokupata, ewe uliyerudi nyuma. Hayo ndiyo yatakayokupata wewe ambaye umemhuzunisha Roho Mtakatifu akaondoka kwako, usiwe mtulivu na mwenye moyo wa upendo tena. Hujalia kwa miaka kadha. Hujatahayari, sijui kwa muda gani, na huna haya kabisa. Hakika. Lakini

yatakujia mlangoni mwako moja ya asubuhi hizi. Na wakati Roho Mtakatifu mtulivu ajapo na kubisha, kwa nini basi usimfungulie mlango?

¹¹⁹ Kwa hiyo Daniel Curry alipofika hapo kwe—kwe—kwenye lango, waliingia, kasema, “Tutaona kama jina lako liko humu.” Wakaangalia kila mahali, hawakuweza kupata jina lo lote. Kasema, “La, hakuna Daniel Curry humu.”

¹²⁰ “Loo,” akasema, “hakika!” Kasema, “Mimi ni mwinjilisti.” Akasema, “Nimewavuta watu kwa Kristo.” Akasema, “Nimejaribu kutenda mema.”

¹²¹ Yule bawabu akasema, “Bwana, ninasikitika kukuambia, lakini hakuna Daniel Curry humu.” Kasema, “Nitakwambia ambalo ungetenda.” Kasema “Sisi hatuna haki hapa ya kushughulikia kesi yako.” Akasema, “Lakini unataka kukata rufani? Waweza kukata rufani kwenye Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi, ukitaka.” Lakini akasema, “Hatuna rehema hapa kwa ajili yako, kabisa, kwa sababu hatukuoni humu. Hutapata rehema.” Kasema, “Unataka kukata rufani?”

Akasema, “Bwana, nifanyeje isipokuwa kukata rufani?”

¹²² Akasema, “Vema, basi, wewe nenda kwenye Hukumu ya Kiti Cheupe cha Enzi ukakate rufani huko.”

¹²³ Daniel Curry alisema kwamba alijisikia akienda angani kwa kama saa moja. Kasema alifika mahali fulani, ikawa mwanga zaidi, zaidi, zaidi, zaidi. Kasema, kadiri alivyozidi kwenda mbele, ndivyo ilivyozidi kung’aa zaidi. Ilikuwa inaangaza mara mia zaidi, mara elfu nyingi kuliko jua lilivyowahi kuangaza. Naye akasema alikuwa akitetemeka, akitetemeka. Kisha akasema, alipofikia katikati ya Nuru ile, alisikia Sauti ikisema, “Ulikuwa mkamilifu duniani?” Ilitoka tu kutoka ka—katika Nuru.

Akasema, “La, sikuwa mkamilifu,” akaanza kutetemeka.

Ikasema, “Ulikuwa mwaminifu sikuzote kwa kila mtu?”

¹²⁴ Kasema, “La.” (Kasema, “Mambo machache yakanijia bongoni ambayo sikuwa mwaminifu hasa kwayo.”) Akasema, “La, na—na—nadhani sikuwa mwaminifu.”

Kasema, “Ulisema kweli katika kila jambo, maishani mwako?”

¹²⁵ Kasema, “La. Nakumbuka baadhi ya mambo ambayo nimesema, ambayo hayakuwa ya hila . . . yaliyokuwa ya hila. Sisi—si—sijapata kuwa wa haki kabisa.”

¹²⁶ Kasema, “Basi, uliwahi kuchukua kitu cho chote kisichokuwa mali yako, kitu cho chote, fedha, kitu cho chote kingine ambacho hakikuwa mali yako?”

¹²⁷ Kasema aliwaza duniani kwamba alikuwa mzuri sana, lakini alihukumiwa. Kasema, “La. La, nimechukua vitu ambavyo havikuwa mali yangu.”

Akasema, “Basi hukuwa mkamilifu.”

Akasema, “La, sikuwa mkamilifu.”

¹²⁸ Akasema alikuwa akitazamia wakati wo wote mlipuko mkubwa utoke kwenye Nuru ile kuu ambapo yule Hua alistarehe, “umehukumiwa!” Kasema, mara akasikia Sauti nyuma yake, ambayo ilikuwa tamu kuliko sauti ya mama ye yote aliyowahi kusikia. Akasema akageuka aangalie. Na uso wa kupendeza sana kuliko uso wo wote aliowahi kuuona, wenye huruma kuliko uso wa mama ye yote, umesimama mbele yake. Ndipo akasema Yeye alisema, “Baba, Daniel Curry alinitetea Mimi duniani. Ni kweli, hakuwa mkamilifu, lakini alinitetea. Alinitetea Mimi duniani, sasa Nami nitamtetea yeye Mbinguni. Chukua dhambi zake zote ukaziweke juu Yangu.”

¹²⁹ Ni nani atakayekutetea siku ile, ndugu, kama ukimhuzunisha Yeye hata akuache leo? Siwezi kuhubiri zaidi. Na tuinamishe vichwa vyetu.

¹³⁰ Mungu Mpenzi, mpenzi Mwana-kondoo unayekufa, mvumilivu, mnyenyekevu, asiye na kiburi. Ndege walikuwa na viota na mbweha walikuwa na matundu, bali Wewe hukuwa na mahali, na, hata hivyo, u Bwana wa Utukufu! Ulipozaliwa, wao hawakuwa na nguo zo zote za kukuvalisha Wewe. Ee Mungu, nguo zangu basi zanifaa nini? Motokaa zangu basi zanifaa nini? Nyumba yangu nzuri yanifaa nini mimi basi? Vitanifaa nini basi siku ile? Hukuwa na marafiki; hakuna mtu aliyetaka kufanya urafiki Nawe. Hakuna mtu aliyeelekea kukupa msaada. Ulisema kwamba siku ile Wewe utasema, “Nilikuwa na njaa, hukunilisha Mimi. Nilikuwa uchi, hungenivika nguo Mimi.” Yatatufaa nini yote tuliyo nayo siku ile, Bwana? Hebu na tukutetea Wewe, ili kwamba saa ile ijapo nasi tunaingia katika Uwepo Wake, Aliye Na Nguvu Zote, Aliyepo Mahali Pote, Yeye Aliye. . . Ee Mungu, tutakapomsikia Hua yule, na mbawa Zake zimewekwa nyuma kule katika Nuru ile kuu, Hiyo itang’aa katika Umilele wote. Ambapo, Wewe hukaa katika Nuru!

¹³¹ “Nitakapopaswa kusimama pale peke yangu, ndugu yangu ameaga dunia, mchungaji ameaga dunia, mama yangu ameaga dunia, baba yangu ameaga dunia, mke wangu ameaga dunia, watoto wangu wameaga dunia. Ee Mungu, nitafanya nini basi wakati huo, Bwana? Nitafanya nini basi wakati huo? Na hilo laweza liwe kabla ya jua kutua usiku wa leo. Lakini nitafanya nini? Nifanye nini? Ee Kristo, nitakutetea sasa! Nitafanya chaguo langu leo. Nitaacha kuzungumza kuwasengenya watu wengine kabisa. Nitaacha hasira zangu. Nitaacha kutojali kwangu kwote. Nitaacha kila kitu. Ninyoe, Bwana, chukua yote niliyo nayo. Hebu wewe nichukue tu, Bwana. Na—na—nataka

kusimama mahali Pako. Nataka ninyolewe. Nataka uchoyo wote, majivuno yote, kutojali kwote, yote yaondolewe kwangu. Kisha nataka nikutetee, kama mwana-kondoo aliyekakwa manyoya, kukubali kuachana na anasa zote za mambo wanayoita anasa za maisha, dansi zote, tafrija zote, nguo zote chafu, vipodozi, rangi ya midomo, rangi ya makucha, huku kutojali kwote ambako huonekana kama ulimwengu. Ulisema, ‘Hata msiende kama walimwengu. Hata msichangamane na walimwengu. Tokeni kati yao!’ Ee Mungu! Nisaidie, Bwana. Ninyoe leo. Nichukue kama mwana-kondoo na hebu nifanye niwe kimya, nisifungue kinywa changu, nisiseme kitu kuhusu jambo hilo, nisimame tu na kukatwa manyoya.”

¹³² Ee Mungu, jinsi inavyofanya tofauti! Ninakumbuka wakati uliponikata manyoya wakati mmoja, ukamchukua mke wangu, mtoto wangu mchanga, na baba yangu, na ndugu yangu, ukaninyoa vizuri sana. Ingawa hivyo, moyoni mwangu, nilijua ninakupenda Wewe. Jinsi Wewe ulivyonibariki, na jinsi Wewe umekuwa mwema! Yote niliyo mimi, yote ambayo ningeweza kuwa, yote ambayo ningewahi kuwa; ni Wewe, Mungu, ni Wewe. Naungama makosa yangu, naungama yote niliyawahi kutenda au kuwaza. Hebu ninyoe, Bwana, nataka kuwa mwana-kondoo Wako.

¹³³ Si hayo tu, Bwana, bali chukua kila mtu aliye hapa ndani asubuhi hii, kila kondoo, na wale ambao wangetaka kuwa kondoo, wanyoe wote, asubuhi hii, Bwana. Weka miguu yao midogo kwenye vifungo vya Injili. Hebu Roho Mtakatifu na awaongoze katika toba sasa hivi, wajue kwamba wamekuwa wasiomjali Mungu. Yeye na akate na kuondoa kutojali kwote, ulimwengu wote na mambo yote ya ulimwengu. Unyoe mambo yote asubuhi hii, Bwana, ili tuweze kudumu wapole na watulivu mbele Zako, kama Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Tujalie hilo, Bwana.

¹³⁴ Nakupenda. Nataka kwenda, haidhuru kama hali ya hewa ni joto, kama ninajisikia kufanya hivyo au la. Nataka kwenda. Nataka kukutetea Wewe, sababu nataka Wewe unitetee siku ile, useme, “Vema, alinitetea Mimi, Nami sasa nitamtetea.” Ee Mungu, tujalie hilo leo.

¹³⁵ Na wakati kila kichwa kimeinamishwa, na kila moyo umeinamishwa. Sijui asubuhi hii kama kuna mtu hapa ambaye anatambua kwamba alijaribu kufuata njia yake mwenyewe, alifanya mambo haya ambayo haimpasa kufanya, na anajisikia tu asubuhi hii angetaka Bwana amnyoe, na aseme, “Akufanye mwana-kondoo halisi,” tafadhali inua mkono wako. Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu. Mtu mwingine aseme, “Ninyoe, Bwana, ninasimama. Mimi ni kondoo. Hata sitafunua kinywa changu, nakutaka tu Wewe ukate uuondoe ulimwengu wote kwangu.” Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki,

mwanangu mwanamume. Mungu akubariki, bibi. Na Mungu akubariki, dada. “Ninyoe, Bwana.” Dada Gertie... [Mcheza piano—Mh.] Na Mungu akubariki, bibi. Na Mungu akubariki, dada. “Ninyoe sasa, Bwana. Na—nataka mambo yote ya ulimwengu. . . Nataka kukutetea asubuhi hii. Nataka kusimama kama kondoo aliyenyolewa. Nataka mambo yote ya ulimwengu yakatwe yaondolewe kwangu. Nataka kuwa Wako na Wewe uwe wangu. Wewe utanipokea, Bwana, ninapoinua mkono wangu Kwako?” Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, bibi, ninauona wako. Mungu akubariki, ndugu yangu. Mungu akubariki, bibi mdogo. Hilo ni jambo jema. Mungu akubariki nyuma huko, mama. Mungu akubariki, dada. Hiyo ni sawa, kuwa tu mwaminifu. “Ninataka Mungu aondoe yote ambayo hayafanani na Yeye, ubinafsi wo wote nilio nao, kutojali kwo kwote niliko nako. Nataka Yeye aninyoe kabisa, asubuhi hii. Nataka kuwa kama Yeye. Sijali kama hizo ni haki au si haki; sina haki zo zote. Nina haki moja tu, nayo ni, kumjia Yeye. Yeye huchukua mengine yote.”

¹³⁶ Yupo mwenye dhambi hapa ambaye hajawahi kumkiri Kristo, hajaokoka kamwe, nawe unataka kukumbukwa katika sala hii asubuhi ya leo, waweza kuinua mkono wako, rafiki mwenye dhambi? Mungu akubariki. Mwingine inua mkono wako, useme, “Nikumbuke, Ndugu Branham. Mimi si Mkristo, na sijui tu ni wakati gani itanibidi nikutane na Mungu. Na na—nataka kukumbukwa sasa hivi katika maombi, unapofunga.” Vema, utainua mkono wako nipate kukuombea? Yeye anaona. Mungu akubariki, bi mdogo. Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, bwana. Mwingine, “Nataka kuwa, nataka ile. . .”

¹³⁷ Ni wangapi hapa ambao wamerudi nyuma? “Loo,” unasema, “singekubali hilo, Ndugu Branham.” Bali, tazama, kama yule Hua wa uvumilivu ameondoka kwako, ndugu, una kasoro. Kuna kasoro mnaposhindwa kuvumiliana mmoja kwa mwingine. Wakati huwezi kumsamehe kila mtu kutoka kilindi cha moyo wako, haidhuru wamefanya nini au wamesema nini, kama huwezi kuwasamehe kutoka kilindi, Yesu alisema, “Kama hamumsamehi kila mtu makosa yake, kwa mioyo yenu, wala Baba yenu wa Mbinguni hatawasamehe ninyi.”

¹³⁸ Sasa vipi basi, katika hali hii ya hewa yenye joto, vipi kama leo hii Mungu angekuita? Wakati kuna Chemchemi wazi, kanisa tayari, Roho Mtakatifu akiketi hapa katika paa la jengo hili, tayari kushuka chini sasa hivi na arudi moyoni mwako na kukufanya mpole na mwenye amani. “Nifanyeje, Ndugu Branham?” Kuwa mwana-kondoo tu. Roho Mtakatifu atashuka moja kwa moja unapokuwa mwana-kondoo. Bali kama una nia mbaya, wazo—wazo baya, unataka ufanye upendavyo, na

hukubali kuacha jambo hilo, basi Roho Mtakatifu hatakuja kamwe.

¹³⁹ Sasa vichwa vyetu vikiwa vimeinamishwa, sijui iwapo ye yote wenu aliyeinua mkono wake. . . Sasa, Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka Mimi, yuna Uzima wa milele, hataingia hukumuni bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani,” Yohana Mt. 5:24. Bali sasa kama ungetaka kuja madhabahuni, kupiga magoti hapa, na tuombe pamoja mpaka kule kujisikia una utulivu, na amani ulikokuwa nako zamani, au ungetaka kuwa nako, kukujie tena. Wakati tunapoviinamisha vichwa vyetu, wakati tunapoimba, “Damu imebubujika,” nataka mje, mpige magoti na kuomba. Kila mmoja sasa ambaye anataka kuja, piga magoti chini hapa penye vipandio vya madhabahu uombe kwa muda.

Damu Imebubujika
Ni ya Imanweli
Wakioga wenye taka. . .
(Mungu akubariki, ewe bibi, njoo upige
magoti)
Husa. . .

¹⁴⁰ Huku vichwa vyenu vikiwa vimeinamishwa, kama ninavyotumaini mmefanya hivyo mioyoni mwenu. Mnajua nani anayetokea katika marefu ya kanisa asubuhi hii, anayepaswa kukufanya ujionee aibu? Mwanamke mweusi, maskini huyu, vifundo vya mguu vimevimba, nywele zenye mvi, anakwenda zake madhabahuni.

¹⁴¹ Hapa wakati fulani uliopita, mzee mmoja mweusi aliokoka, wakati wa utumwa. Akaenda, naye kwa kuwa ameokoka, alimwambia boshi wake yeye alikuwa huru. Akasema, “Ati nini?”

Kasema, “Niko huru.” Basi akamfanya huru.

¹⁴² Hili hapa kundi jingine la watu likishuka kuja lipate wokovu asubuhi hii. (Kasema alikuwa huru.) Kila mtu awe katika maombi, basi ombeni kwa bidii tafadhali, wakati Roho Mtakatifu anashughulika na watu wanaofanya uamuzi.

Akasema, “Mose, unasema ulikuwa huru?”

Akasema, “Ndiyo, bwana, boshi. Mimi ni huru.”

¹⁴³ Akasema, “Kama uko huru, basi mimi nami nitakufanya huru, pia. Nenda ukahubiri Injili.”

¹⁴⁴ Alipokuwa tayari kufa, wengi wa ndugu zake wazungu wakaja kumwona, na walipokuja, akasema, alifikiri amelala fofofo. Alipoamka, akasema, “Nilifikiri nimeaga dunia.” (Mungu akubariki, ndugu yangu, piga magoti kabisa. Kasema, “Nilidhani tayari nimekwisha kuaga dunia.”

Kasema, “Uliona nini, Mose?”

¹⁴⁵ Akasema, “Nilipoingia malangoni, nilimwona Yeye.” Kasema, “Nilikuwa nimesimama, huku ninamtazama Yeye.” Naye kasema, “Akatokea Malaika akasema, ‘Njoo, Mose. Umekwisha hubiri Injili miaka mingi, joho na taji zinakungoja.’ Akasema, “‘Usinizungumzie kuhusu joho na taji. Sitaki joho wala taji. Nataka tu kumwalia Yeye.” Nafikiri hiyo ndiyo nia ya Mkristo ye yote.

¹⁴⁶ Hapa wakati uliopita, huko juu nje ya Chicago, nilikuwa kwenye jumba la michezo, jumba la makumbusho, hasa, na nilikuwa ninaangalia pande zote mle ndani. Nilimwona mzee wa Kinegro, mzingo mdogo wa mvi kichwani mwake, akitembea humo, ameishika kofia yake mkononi mwake. Nikamwalia. Akaangalia kwenye sehemu ndogo, kisha akaruka nyuma, na machozi yakaanza kutiririkia kwenye shavu lake jeusi lililozeeka. Akaanza kuomba. Nikamwalia kwa muda kidogo. Akaangalia tena, akaanza kulia tena. Nikamwendea na kusema, “Bwana.”

Akasema, “Ndiyo, rafiki yangu mzungu?”

Nikasema, “Naona uko . . . Jambo gani limekusisimua hivyo? Umesisimshwa na nini?”

¹⁴⁷ Akasema, “Bwana, kama ungalinigusa mbavuni, nina sugu ubavuni mwangu.” Kasema, “Hapo kwanza mimi nilikuwa mtumwa.” Akasema, “Katika hiki kizimba kidogo hapa cha kioo, ile ni nguo imewekwa mle.”

Nikasema, “Naona ni nguo, lakini ina umaalumu gani?”

¹⁴⁸ Akasema, “Hiyo alama pale,” akasema, “hiyo ni damu ya Abraham Lincoln.” Akasema, “Damu hiyo ilinifungua kamba ya utumwa.” Akasema, “Sasa, ewe mzungu, je, kwa namna fulani si ingekusisimua wewe pia?”

¹⁴⁹ Nikamkumbatia shingoni, nikasema “Mungu akubariki, ndugu. Ninajua Damu nyingine inayonisimua.”

Akasema, “Najua Damu, hiyo pia, bwana.”

¹⁵⁰ Nikasema, “Yeye alinifungua kamba ya utumwa.” Wakati mmoja ningetoka Jumapili na kukimbia na kufanya yasiyofaa, na kutania utani mbaya. Na, Ee Mungu, nilitenda hivyo jinsi gani? Bado kuna kovu moyoni mwangu nilikoitenda. Lakini nina furaha Yeye alinifungua ile kamba. Zote zimeondoka sasa, Yeye alisimama mahali pangu.

¹⁵¹ Hapa wakati uliopita, nikimwalia mwanamke, naye alikuwa mtovu sana wa adabu hata nilitaka kumhukumu. Basi Mungu akanipa ono. Nikamwomba basi, kwani niliona kwamba dhambi zangu zilikuwa kubwa kama zake. Nami nilienda nikaketi karibu naye na kumwaibisha, nikamwambia nilikuwa mhudumu. Marafiki zake wawili wa kiume . . . Alikuwa na yapata umri wa miaka sitini na mitano au sabini, rafiki zake

wawili wa kiume walipiga magoti pale, nao wote wakatoa mioyo yao kwa Kristo. Loo, jamani, ni tofauti jinsi gani!

¹⁵² Na wewe je? Umekwisha tenda dhambi sana, asubuhi hii, umefanya moyo wako kuwa mweusi sana na mchafu mpaka hata Roho Mtakatifu hawezi hata kuugusa? Pengine Hua ameruka akaenda Zake Milele, amekwenda kabisa.

¹⁵³ Mungu akubariki, mpenzi. Msichana mdogo anakuja. Mungu akubariki, kipenzi. Unasema, “Huyo msichana mdogo hajui.” Loo, ndiyo, anajua. Hajasoma tu magazeti mengi na hadithi nyingi za kale za mapenzi kama mliyosoma ninyi nyote. Hiyo ndiyo shida, si mgumu. Yesu alisema, “Waacheni watoto wadogo waje Kwangu.”

¹⁵⁴ Kuna mtu mwingine ambaye angetaka kuja, ajiunge hao hapa asubuhi hii? Madhabahu yako wazi. Hebu kidogo tena, ndipo basi wakati tunaimba mara nyingine, basi tutafanya maombi wakati hawa wenye dhambi wanaotubu wanaomba.

Ilimpa kushukuru
Mwivi mautini... (Hakika, kila kitu
kimekwenda, maskini jamaa yule
amekwisha)
Nami nisiye udhuru,
Yanisafi ndani

¹⁵⁵ Mbona usije huku sasa? Mbona usije huku, wewe ufahamuye vyema zaidi? Biblia ilisema, “Kama unajua kutenda mema, nawe usitende, kwako ni zaidi ya dhambi.” Je, mbona usije? Unajua umekosea. Njoo huku upige magoti madhabahuni, unwambie Mungu unasikitika kwa yale uliyomtenda Yeye. Mruhusu Roho Mtakatifu arudi akufanye mpole na mtulivu na mnyamavu tena. Utamruhusu? Kumbuka, kama ukifa, na Yeye amekuacha, hakutakuwa na mtu wa kukutetea. Yeye anataka umtetea asubuhi hii. Mungu akubariki, ndugu yangu.

¹⁵⁶ Nangojea. Je, ni hawa tu, watu kumi na watano tu kanisani ambao kweli wanajiona wamehukumiwa? Umeishi maisha yaliyojaa amani, ya upole, ya utulivu, unyamavu? Sasa, hili linaongozwa na Roho Mtakatifu. Wewe husamehe, huna adui? Unaishi kupita juu ya hukumu ya wenye dhambi? Huishi kama makafiri, unaishi tofauti? Je, maisha yako yana mfano tofauti? Je, Roho Mtakatifu aliye mtulivu anaketi juu ya kiti cha enzi cha moyo wako, akikufanya uishi kwa amani na utulivu na mwenye upendo, miongoni mwa watu wote? Je, majirani zako na wengine wote wanajua, na wote unaochangamana nao wanajua, kwamba u Mkristo, mtulivu, mnyamavu, mpole, mnyenyekevu? Je, Hua wa Mungu yu pamoja nawe? Una hakika? Hii yaweza iwe nafasi yako ya mwisho. Vema.

¹⁵⁷ Basi kwenu ninyi mlio hapa madhabahuni, Mungu awabariki. Haitawapasa kuhukumiwa sasa. Roho Mtakatifu ameleta hukumu kwenu. Na hamkujaribu kushikilia haki

zenu, kusema, “Loo, nimekuwa Mkristo muda mrefu sana vya kutosha. Hainilazimu kwenda pale.” Baadhi yenu, ni mara yenu ya kwanza kuwa madhabahuni. “Naweza kubakia mwenye dhambi nikitaka, hiyo ni haki yangu.” Ndiyo, hilo ni kweli. U kiumbe huru, waweza kutenda unayotaka. Bali ulipoteza haki zako asubuhi hii. Wasema, “Watasemaje, mimi ninayekiri Ukristo nikienda madhabahuni, watasemaje?” Lakini Mungu anasemaje? Alisema wewe uje, na umefanya hivyo. Sasa ulipoteza haki zako, umekuja kumfanya Roho Mtakatifu aliye mtulivu achukue mahali Pake moyoni mwako leo. Najua Yeye atafanya hivyo. Najua atafanya. Yeye aliahidi atafanya hivyo. Hapo, Yeye hawezi kamwe kujizuia, hawezi kujizuia kuja. Yeye anasihi, analia, alikufa, na kadhalika, apate mahali pa kuingia, akitaka kuja kwako.

¹⁵⁸ Na katika saa zako za kufa, wakati malaika wa kifo anaketi kwenye mguu wa kitanda, badala ya kuangalia nje uone jambo la kutisha, na kujua kwamba ulikataa kuja wakati mmoja, na kisha nafsi yako inakuwa nyeusi na chafu, hakuna wakati mwingine, haidhuru ulilia kiasi gani. Esau alitenda dhambi akamaliza dhambi yake ya neema... akamaliza siku yake ya neema, hasa, naye hakupata nafasi. Alilia kwa uchungu, akijaribu kutafuta nafasi ya kutubia, bali hakuweza kufanya hivyo. Mungu alimwita mara ya mwisho.

¹⁵⁹ Lakini unapoteza haki zako zote na rafiki zako wote, na kujisikia kwako kwote na kila kitu, asubuhi hii, kuja hapa. Ulipoteza haki zako, kupiga magoti hapa na kuzungumza na Mungu. Ninakuambia kwa Neno la Bwana, kwamba Kristo alisema, “Yeye ajaye Kwangu, sitamtupa nje kamwe.” Sasa huku ukiwa hapo madhabahuni, tubu, mwambie Yeye kwamba unasikitika ulitenda uliyotenda.

¹⁶⁰ Hiyo ndiyo sababu watu hawapokei Roho Mtakatifu wanapobatizwa, hawatubu kikamilifu. Mungu anajaribu kuwapa Roho Mtakatifu. Anataka wewe uwe mpole na mtulivu, mnyamavu. Hiyo ndiyo sababu unainuka na uchoyo ule ule moyoni mwako. Loo, unaweza kuinuka, ukipaza sauti kwa nguvu, ukivena kwa lugha, au cho chote, hilo lisingekufanya uwe na Roho Mtakatifu. Yakubidi uinuke utoke hapo ukiwa mtu tofauti. Yakubidi uamke utoke hapo mtulivu, mnyamavu na mpole, mnyenyekevu, na Roho wa Mungu akikaa pamoja nawe. Mwaka ujao, tazama nyuma ulikopitia uone umbali gani umekuja, utaona unasonga mbele wakati wote. Huyu ni Roho Mtakatifu. Roho Mtakatifu ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, upole, utu wema, saburi, imani. Sasa, hebu tubu tu na umwambie Mungu unataka hilo sasa hivi. Yeye atalitenda.

¹⁶¹ Ewe msichana mdogo, wewe pale, kipenzi, fanya jambo lilo hilo. Ubarikiwe. Mama yako akisimama na mikono yake juu yako.

¹⁶² Huyu dada mpendwa mzee mweusi hapa, anayeinama madhabahuni. Pengine ilikubidi kula mkate wa mahindi na biskuti za mahindi, pengine imekubidi kuishi vichochoroni, nijuavyo mimi, dada. Mungu aubariki moyo wako, kuna jumba la kifalme uliloandaliwa huko Utukufuni asubuhi hii. Sawa.

¹⁶³ Naangalia kule chini madhabahuni na kumwona bibi, akianza kupata mvi, kijana mwanamke ameinamisha kichwa chake chini, mwanamke aliyejaa mvi. Ee Mungu! Angalia mtu anayepiga magoti, watu mbalimbali hapa. Hebu tubuni tu, mwambie Yeye unasikitika. Mwambie Yeye hutafanya jambo hilo tena. Kwa neema Yake, utaacha tu tofauti zako zote ziishe, tangu leo. Unataka kuwa mtulivu na mnyamavu. Unataka kuwa mnyenyekevu na kwenda ambako Yeye anakuongoza.

¹⁶⁴ Watu wanaposema kitu, haidhuru inaonekana ni kweli jinsi gani, utaacha haki zako kuzungumza kuhusu jirani yako. Utazungumza, utazungumza juu ya Yesu. Utatenda tu jambo ambalo ni sahihi. Hutaondoka uende kama muuaji. Hutarukia wasio na hatia. Bali unaona onyesho lile nzuri la kishujaa la Wakristo wa kweli, nawe unataka kuwa kama wao. Haitakulazimu kumwambia mtu ye yote wewe u Mkristo, kama ndivyo ulivyo, watajionea tu na kujua hivyo unapozungumza. Umetiwa muhuri ndani na nje.

¹⁶⁵ Sasa, wakati unaponyenyekea kwa moyo wako, tubu sasa. Mwambie Mungu “unasikitika,” wewe “hutamifanya tena,” unajionea “aibu,” mwenyewe, namna ulivyotenda. Ndipo nitakuombea. Nami naamini, papo hapo, amani itakaa moyoni mwako, amani tu kama mto itakuja ikitiririka nafsini mwako. Huenda ikawa haupazi sauti, huenda ikawa huneni kwa lugha, huenda ikawa huruki juu chini; bali utaondoka madhabahuni na Kitu ndani yako, Kitu ndani yako ambacho kitakuweka nanga kwenye ule msalaba wa kale unaoparuza maadamu ungali hai. Sasa omba, ninapomba. Ungama.

¹⁶⁶ Baba yetu wa Mbinguni. Viumbe visivyostahili, chumba hiki chenye joto, na jasho asubuhi hii, hili sanduku la jasho; bali, Mungu, Wewe ulitoa jasho kwa ajili yetu. Roho Mtakatifu alishuka, akawathibitishia watu kwamba wana hatia. Walikuwa wanatenda dhambi. Roho zao zilikuwa zenye kiburi. Wamekuwa na chuki, vilimilimi, vimbelembele, wasiokubali kutubu, wasiokubali kuwasamehe waliowakosea. Hawakuwa wanakubali kuwasamehe, bali leo Roho Mtakatifu amelichukua Neno la Mungu, akaliweka moja kwa moja kwenye mioyo yao mitulivu, na akasema, “Sasa unataka kurudi mahali ambapo ulikuwa mara ya kwanza ulipokuja madhabahuni, urudi ambapo kila mtu, unampenda kila mtu, na unanipenda Mimi kwa upendo unaodumu? Basi inuka tu uje madhabahuni.” Wamefanya hivyo, Bwana.

167 Sasa, naomba sasa kwamba Wewe utatakasa mawazo yao, Bwana; takasa mioyo yao na uwafanye watulivu na wenye amani. Hebu na wainuke kutoka katika madhabahu haya sasa, baada ya wao kutubu, wakiyatoa maisha yao Kwako, warudi nyumbani mwao. Haidhuru jambo gani linatukia, kama mume akikasirika, au mke akikasirika, au jirani akikasirika, au mtu fulani ambaye unafanya kazi naye au kushirikiana naye, “Nitakuwa tu mtulivu kama hua.”

168 Hata hivyo, kisasi Chako ni juu Yako, “Mimi nitalipa, asema Bwana.” Jinsi tumeona jambo hilo kuwa ni kweli, Bwana. Simama tu kimya, tulia, muone Mungu akichukua . . . akija moja kwa moja kwa mwana-kondoo Wake. Hakika, bila shaka. Huyu Mchungaji mwema alitoa Uhai Wake kwa ajili yao. Alishuka akaja moja kwa moja kwa kondoo Wake. Naye atawaongoza. Ole wake yule anayewaudhi! Ole wake yule ambaye ananena neno moja dhidi yao! Kasema, “Yafaa ufungiwe jiwe la kusagia shingoni mwako, na kutoswa katika kilindi cha bahari. Malaika zao sikuzote huuangalia uso wa Baba Yangu aliye Mbinguni.” Unaona? Ee Mungu, tunataka . . . “Na kadiri muwatendeavyo hao, mnanitendea Mimi.”

169 Kwa hiyo, Mungu, nataka kuwa mtulivu. Najiweka mwenyewe madhabahuni, pia, asubuhi hii, si asubuhi hii, bali kila asubuhi na kila siku. Nataka kuwa mnyamavu na mtulivu, kama Yesu. Lijalie, Baba. Tusaidie kuwa hivyo sasa, ruhusu mawimbi ya upendo yasiyopimika kina yafunikize nafsi yetu.

Amani! Amani! Amani ya ajabu,
Ishukayo kutoka juu kwa Baba;
(Je, huisikii Hiyo sasa katika mioyo yetu?)
. . . juu ya roho yangu sikuzote, (Haleluya!
Haleluya!)
Amani! Amani! Amani ya ajabu!

170 Dada Gertie amesema kanisa lote liambiwe yeye amehukumiwa, pia, bali anafanya piano kuwa madhabahu yake. Kwa vile madhabahu, piano ndiyo madhabahu yake, kasema, “Liambie kanisa liniombe,” anapoketi pale na huku machozi yanatiririka chini ya miwani yake. Mimbara hii ni madhabahu yangu. Nimetubu, pia, Biblia yangu imelowa. Ee Mungu!

Amani, amani ya Mungu!
Ishukayo kutoka juu kwa Baba; (Ee, haleluya)
. . . juu ya roho yangu sikuzote.

171 Mungu, kama nimemtenda mtu ye yote dhambi, dhidi Yako, iondoe, Bwana. Ondoa dhambi kwenye kanisa langu dogo asubuhi hii.

172 Ni wangapi wanaweza tu kujisikia kwamba Mungu amekusamehe, na Hua wa Amani anaketi katika moyo wako tena? Ameruka akarudi tena sasa hivi, akachukua mahali Pake. Roho Mtakatifu ndiyo kwanza arudi na kusema, “Mwanangu,

nimekuwa nikitaka kukupenda wakati wote. Hungeniruhusu Mimi kufanya hivyo. Siwezi kukaa na roho yako ya kale yenye choyo. Bali sasa kwa kuwa umeitoa, Mimi nimerudi moyoni mwako asubuhi hii.” Wangapi wanaojisikia jinsi hiyo, inueni mikono yenu? Inueni mikono yenu, hiyo ni sawa, kote madhabahuni. Loo! hilo ni zuri. Ni wangapi wanaojisikia hivyo katika mkutano huu? Inua mkono wako. Loo! [Ndugu Branham anamwambia mpiga piano, “Kuwa Kama Yesu”—Mh.]

¹⁷³ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa wakati huu mzuri wa kujiweka wakfu, kama vile kuchukua tofaa mkononi, kulipondaponda, kulitwanga tu, mpaka linakuwa laini, laini sana hata mtoto mchanga angeweza kuketi chini na alile. Hivyo ndivyo tutakavyo mioyo yetu, Bwana. Uchukue katika mkono Wako ulio na kovu la misumari, ukautwange, ukisema, “Mwanangu, huoni umeniudhi Mimi? Ulikuwa unaniudhi Mimi wakati ulipokuwa unakosa kutawala hasira zako jinsi hiyo. Ulikuwa unaniudhi Mimi, loo, Mimi nilikuonea huruma sana, mwanangu, nilipoona unafanya mambo haya na yale. Bali sasa nimeushika moyo wako mkononi Mwanangu, nataka kuufanya mpole kweli. Nataka kuufanya hivi kwamba naweza kuutumia na kuishi ndani yake. Nataka niruke kurudi kwenye kiota asubuhi hii, nataka kuruka nirudi na kuketi, kufanya makao Yangu pamoja nawe.” Tujalie, Ee Mungu. Tunakupenda. Tujalie, kwa ajili ya utukufu Wako. Twaomba katika Jina la Yesu.

Kuwa kama Yesu, ku . . . (Hupendi tu kuabudu jinsi hii? Loo, nafsi yangu inaogelea tu.)
 Duniani na . . . (Kumuona Yeye akishuka na kuingia ndani ya—ya waabuduo jinsi hii, moyo wako unajisikia mtulivu kabisa? Moyo wangu unapigapiga tu haraka.)
 . . . safari yote toka duniani hadi Utukufuni.
 Naomba tu kuwa kama Yeye.

Waweza kuinua mkono wako tunapouimba?

Kuwa kama Yesu, ku . . .
 (Joe, unataka kuja kuomba asubuhi hii, ndugu? Mungu akubariki. Jitafutie mahali hapa madhabahuni, Ndugu Joe. Mungu akubariki.)
 . . . safari yote toka duniani hadi Utukufuni
 Naomba tu kuwa kama Yeye.

¹⁷⁴ Najua kuna joto, enyi marafiki. Najua kuna joto. Lakini na—natumaini mnajisikia tu kama vile ninavyojisikia. Loo, najisikia tu kama ningeweza tu kuruka niende zangu. Jinsi Yeye alivyo na upendo! Ningefanyaje? Ningeenda wapi? Ee Mungu! Ninaenda wapi? Ninaelekea wapi? Itakuwa—itakuwaje? Nitakuwa wapi

miaka mia moja tangu sasa? Vipi kama sikuwa Naye? Liko, liko wapi kimbilio jingine?

Toka hori la Bethlehemu alikuja Mgeni,
Duniani natamani kuwa kama Yeye.
Katika safari yote ya maishani toka duniani
hadi Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.

Wote pamoja sasa.

Kuwa kama Yesu. . . (Mungu atukuzwe! Ndiyo,
Bwana! Ndiyo, Bwana! Si ulimwengu; kama
Wewe!)
. . . kuwa kama Yeye;
Katika safari yote ya maishani toka duniani
hadi Utukufuni
Naomba tu. . .

¹⁷⁵ Wakati mmeinamisha vichwa vyenu, nitawaulizeni jambo fulani. Mtu fulani ndani hapa anamhuzunisha Roho Mtakatifu. Mtu fulani amekwisha kuitwa. Nanena katika Jina la Bwana Yesu, kama nabii Wake. Naweza kuhisi moyo Wake umejeruhiwa. Ndani huko, mtu fulani amemkaidi Yeye, aliyepaswa kuja. Mbona usije sasa?

Katika safari yote ya maisha toka. . . (Ndiyo,
dada, lakini wapo zaidi ya wewe). . .
Utukufuni
Naomba tu kuwa kama Yeye.
Kuwa tu kama Yesu. . . (Hiyo ndiyo hamu
yangu yote, kuwa mpole, mnyonge,
mnyenyekevu, kuwa kama Yeye)
Duniani na. . . (Mbona usije sasa? Mungu
anataka kukuona ukijimudu, kuna baadhi
yenu)
Katika. . .

¹⁷⁶ Nilijua mlikuwa mnakuja, Mungu akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Ndiyo. Ndiyo. Niliangalia kote katika kusanyiko hili, na kivuli cheusi na kibaya sana nilichopata kuona kinaning'inia pale. Roho Mtakatifu yupo hapa sasa. Yuko juu yangu sasa hivi. "Kumhuzunisha Roho Mtakatifu."

Kuwa kama Yesu. . .

¹⁷⁷ Yeye alifanya nini? Alikwenda ambako Baba aliongoza. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki, ndugu yangu. Hilo ni kweli, njoo moja kwa moja huku na piga magoti.

Duniani natamani. . .

¹⁷⁸ Sasa ndio wakati wa maungamo ya kikale, kujiweka sawa, kutengeneza. Njoo. Bado najisikia kuna wengine zaidi humo ndani. Mungu akubariki, bibi. Mungu akubariki, bibi. Mungu

akubariki. Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni sawa. Roho Mtakatifu sikuzote ni sahihi. Njoo. Hilo ni sawa, tokeni.

Yeye, kuwa kama Yesu, kuwa kama, ndiyo, Yesu,

Duniani na... (Loo, jamani, hiyo ni kweli! Ndivyo hivyo, jazeni tu marefu ya kanisa, tokeni humo na muombe)

Katika safari yote ya maisha toka duniani hadi Utukufuni, (Tubu tu, mwambie Mungu unasikitika, hilo tu ndilo likupasalo kutenda) ...kuwa kama Yeye.

¹⁷⁹ Tafadhali endeeleni kuja sasa. “Ku...” Hilo ni sawa, hebu jiachilie, njoo. “Kuwa kama...”

¹⁸⁰ Utafanya nini? Utatetewa na nani, pengine usiku wa leo? Utatetewa na nani wakati mauti yatakapokukaribia? Haidhuru umefanya nini, Roho Mtakatifu amekaa papo hapo karibu nawe. Huyu Ndiye anayetaka uje.

Katika safari yote ya maisha toka duniani hadi Utukufuni.

¹⁸¹ Hebu tubu tu, useme, “Mungu, ninasikitika. Si—singetaka kufanya jambo hilo. Hutanitetea nisipokutetea Wewe sasa. Nami nataka Wewe unitetee, nami nitakutetea Wewe tangu leo. Nitaishi kama impasavyo Mkristo kuishi. Nitabadilisha mwenendo wangu. Nitakuwa mtu mtulivu na mnyamavu. Nitamwacha kila mtu azungumze atakavyo, kila kitu. Nitaishi tu mpole na mnyamavu mbele Zako.” Haidhuru umekiri kuwa Mkristo muda mrefu jinsi gani, u wa kanisa gani, hayo ni mamoja. Njoo. Mungu akubariki. Toka moja kwa moja, mwanangu.

¹⁸² Mungu anazungumza na wewe sasa. Kama unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, Roho Mtakatifu alizungumza nami asubuhi hii, kasema, “Fanya mwito huo, wako wengi kule.” Siku ndiyo hii, wakati ndio huu. Kuna kama watano au sita zaidi nyuma kule, kwa kweli wanapaswa kuja sasa. Kumbuka, ndugu, dada, ninakuangalia moja kwa moja, ninaona hivyo vivuli vyeusi vikining’inia juu yako. Afadhali uje moja kwa moja.

¹⁸³ Kuwa kama Yesu! Je, hutaki kuwa kama Yeye, mtulivu, mnyamavu, mpole, mnyenyekevu? Mungu akubariki, kijana. Mungu akubariki, baba uliyemshika mtoto. Mungu akubariki dada. Mungu akubariki, rafiki mwenye dhambi. Hilo ni kweli. Njoo huku, dada, toka uje, jitafutie nafasi. Mungu akubariki.

¹⁸⁴ Dada mpenzi, una mengi ya kutolea shukrani. Ulikuwa huwezi kitandani, ukifa, nawe hapa unakuja madhabahuni. Mungu na abariki moyo wako mwororo.

¹⁸⁵ Roho Mtakatifu akizungumza tena sasa. Toba, hebu mlilie tu Mungu, omba tu sala yako mwenyewe. Wewe ndiwe uliyefanya

dhambi, sasa wewe ndiwe unayeomba. Mwambie Mungu unasikitika kwa yale uliyotenda. Usijali ni nani yuko karibu nawe. Sema tu, “Mungu, nisamehe, sikutaka kuwa namna hiyo. Nataka kuwa mtu mwema. Nita—sitashikwa na hasira kamwe wala kugombana tena.”

¹⁸⁶ Ee Mungu, loo, jinsi ninavyopendezwa! Baba wa Mbinguni, kwa ajili ya kila mmoja anayetubu hapa madhabahuni sasa, wakipiga magoti, wakiomba! Ee Mungu, hebu akina mama, baba, watoto, baba, mama, ye yote yule, majirani, washiriki wa makanisa, mashemasi, wadhamini, Ee Mungu, kwenye wakati huu wa mtindo wa kizamani wa kufinyangwa, huku tumeketi katika chumba hiki chenye joto asubuhi hii, Roho Mtakatifu akishuka moja kwa moja, akizungumza amani. Ee Mungu, nataka kusimama siku ile nikusikie Wewe ukisema, kwa upole, “Ndiyo, ulikuja ukanitetea Mimi, sasa Mimi nitakutetea.” Nakuomba Wewe uweke amani ile katika kila moyo ambao upo hapa leo, Mungu. Kwa unyamavu na kwa utulivu, nakuomba Wewe ufanye hivyo. Nakuomba Wewe uingie mle ndani wakijisikia kwamba haitawaacha tena, tangu leo. Nyumba na ziwe mpya. Watu na wawe watu wapya. Kila kitu na kiwe kipya leo, kwa sababu watu hawa wamejinyenyekeza. Wewe ulisema, “Ikiwa watu walioitwa kwa Jina Langu watajinyenyekeza, na kuomba, basi nitasikia toka Mbinguni.” Nami najua Wewe unasikia, asubuhi hii, Mungu.

¹⁸⁷ Pia naomba msamaha kwa wale ambao walibakia kwenye viti vyao, ambao wangepaswa kuja. Mungu, nena nao, nao na wasiwe na amani tena duniani mpaka wamefanya uamuzi ule, Bwana, kuja na kujipatanisha na Wewe. Tujalie, Bwana. Mbariki kila mmoja sasa. Wema Wako na rehema Zako zikae juu ya kila mtu ambaye ametubu na ameinama chini katika kanisa hili asubuhi hii.

¹⁸⁸ Baba, Mungu, nimetenda hili kwa agizo Lako. Nimewaita watu hawa; wamesimama. Wewe ulisema, “Yeye ambaye atanishuhudia Mimi mbele ya mtu, huyo nitamshuhudia mbele ya Baba Yangu na Malaika watakatifu.” Wengi wa watu hawa hapa wamekuwa Wakristo kwa miaka mingi, lakini wanasimama asubuhi hii kushuhudia dhambi zao kwamba wametenda makosa. Wamekuwa wasiopendeka. Roho Mtakatifu ameondoka kwao. Na wakati mwingi hawawezi kuwa na ile hisi ya utulivu, furaha, na upole ambayo wanapaswa kuhisi. Wengi wao ni wenye dhambi ambao wamekuja kwa mara yao ya kwanza. Bali, Baba, wanataka kule kujisikia kwa ajabu, amani ipitayo akili zote. Wape hiyo siku hii, Bwana Mungu, na wawe kabisa kabisa watu wa kupendeza na wajawe na Roho Wako, wanapoondoka mahali hapa leo, waende kila mtu nyumbani kwake, wakaishi maisha tofauti na wawe watu tofauti. Twaomba haya katika Jina la Kristo.

189 “Nafasi Kwenye Chemchemi.” Sawa, ninyi mlio madhabahuni, simamemi, mtazameni Bwana Mungu, geukeni mkapeane mikono na kila mmoja aliye karibu nanyi. Loo, tutaimba, kila mmoja sasa, wakati tunasimama kwa muda tu kabla ya ibada ya kuponya.

Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;

Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako; (Kila mmoja!)


Nafasi, nafasi, naam, kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako;

Nafasi, nafasi, ndiyo kuna nafasi,
Kuna nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili
yako.

Nafasi, nafasi, naam kuna nafasi!
[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

190 Imani! Unajua juzi juzi, ndugu, wakati mke—mke wako alipiga simu, kwamba uombewe? Niliingia moja kwa moja chumbani, na Roho Mtaktifu akaniambia, “Usiogope.” Amina. Je, Yeye si ni halisi? Ajabu! Vema, Bwana asifiwe! Najisikia tu kama nataka kupiga ukelele wa ushindi! Sawa.

Na Damu Yake husafisha ikawa nyeupe
zaidi. . . (Sema kitu Ndugu)
Yesu huokoa!

191 Sawa, Ndugu Neville sasa. Na Ndugu Slaughter anataka kusema kitu. [Ndugu Slaughter anazungumza—Mh.] Bwana asifiwe! [Ndugu Neville anasema, “Naamini kila mmoja amepokea asubuhi hii.”] Utukufu! Haleluya! Haleluya! [Ndugu Neville anazungumza, kisha anasema, “Kumbukeni ibada usiku wa leo, tuna kutawadhana miguu na ibada ya meza ya Bwana.” Anamuuliza Ndugu Branham, “Je, una habari kama utakuja humu?”] Pengine nitakuwa hapa usiku wa leo, pia. Ndiyo, kadiri ni juavyo, nitakuwa hapa nisipoitwa nje mahali fulani. 

Kanisa Halisi
(*The Church*)

Jumbe hizi za Ndugu William Branham, zilihubiriwa hapo awali katika Kiingereza kwenye Maskani ya Branham kule Jeffersonville, Indiana, Marekani, zilitolewa kwenye kanda za sumaku na kupigwa chapa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2009.

SWAHILI

©1991 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org